# UHAKIKI WA HALI YA VIJANA KATIKA RIWAYA YA *VIPANYA VYA MAABARA*

NA

**RUTH NALIAKA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

University of NAIROBI Library
0389600 8

**2012**

## UNGAMO

**Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.**

Naliaka ____________________ 2/11/2012 ____________________

RUTH NALIAKA Tarehe

MTAHINIWA

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi

____________________ 05.11.2012 ____________________

DKT. NYACHAE MICHIRA Tarehe

MSIMAMIZI

Jerono ____________________ 6/11/2012 ____________________

DKT. PRISCA JERONO Tarehe

MSIMAMIZI

## TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wanangu Brian, Bramwel na Elvira kwa kunihamasisha nijitahidi kuboresha masomo yangu katika utu uzima.

# YALIYOMO

**UKURASA**

SHUKRANI ........ iv
MUHTASARI ........ v
SURA YA KWANZA ........ 1
1.0 Utangulizi ........ 1
1.1.Tatizo la Utafiti ........ 3
1.2 Madhumuni ya Utafiti ........ 4
1.3. Natharia Tete ........ 4
1.4. Sababu za Kuichagua Mada Hii ........ 4
1.5. Upeo na Mipaka ........ 5
1.6. Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ........ 6
1.7. Msingi wa Kinadharia ........ 7
1.8. Njia za Utafiti ........ 11
SURA YA PILI ........ 12
UHUSIKA ........ 12
2.0 Utangulizi ........ 12
2.1. Dhana ya Uhusika ........ 12
2.2. Uainishaji wa Wahusika ........ 15
2.3. Aina za Wahusika ........ 16
2.4. Wahusika Wakuu ........ 16
2.5. Wahusika wasaidizi au wajenzi ........ 17
2.6. Wahusika wa Miraba Minne na wa Mraba Mmoja. ........ 19
2.7. Wahusika Jumui ........ 20
2.8. Wahusika wa Kimapinduzi ........ 20
2.9. Wahusika wa Kisaikolojia ........ 21
2.10. Wahusika wa Kiupelelezi ........ 22
2.11. Wahusika Duara, Bapa na Shinda ........ 23
2.11.1 Wahusika Duara ........ 23
2.11.2 Wahusika Bapa ........ 24
2.11.3. Wahusika Shinda ........ 25
2.12. Wahusika Vijana ........ 25
2.13. Wahusika Viongozi ........ 26

2.14. Wahusika Wazazi ........ 26
2.15. Wahusika Vinyago au Kerekecha ........ 27
2.16. Mhusika wa Kihalisi ........ 27
2.17. Hitimisho ........ 28
SURA YA TATU ........ 29
UHAKIKI WA WAHUSIKA ........ 29
3.0. Utangulizi ........ 29
3.1. Bob Kerogo ........ 30
3.2. Vera ........ 33
3.3 Wairi ........ 36
3.4. Jamila ........ 38
3.5. Freda ........ 40
3.6. Swaleh ........ 42
3.7. Muli ........ 43
3.8. Okach ........ 44
3.9. Konstebo Kerogo ........ 45
3.10. Mama Maria ........ 46
3.11. Waziri Rashid Hamisi ........ 48
3.12. Kamash ........ 49
3.13. Seneta King ........ 50
3.14. Mjomba Mbaabu ........ 51
3.15. Devji ........ 51
3.16. Mama Kegonda ........ 52
3.17 Mwalimu Ramadhani na Mkewe ........ 52
3.18. Inspekta Fadhili na Mkewe/ Sajini Njoroge na Mkewe ........ 53
3.19 Mwalimu Nyamboki ........ 54
3.20. Hitimisho ........ 54
SURA YA NNE ........ 56
UHAKIKI WA MAUDHUI KUHUSU VIJANA ........ 56
4.0. Utangulizi ........ 56
4.1. Ukosefu wa Malezi Bora ........ 56
4.2. Matatizo ya Madawa ya Kulevya ........ 61
4.3. Umaskini ........ 65
4.4. Ukosefu wa Ajira ........ 67

4.5. Ukosefu wa Maadili ........ 70
4.6. Maradhi ya Ukimwi ........ 73
4.7. Ufisadi ........ 74
4.8. Vijana kutumiwa kama Vipanya vya Maabara. ........ 75
4.9. Vijana kama msingi wa kubomoa ukabila ........ 76
4.10. Hitimisho ........ 77
SURA YA TANO ........ 78
HITIMISHO LA UTAFITI ........ 78
5.0 Utangulizi ........ 78
5.1. Matokeo ya Utafiti. ........ 78
5.2. Mapendekezo ........ 79
MAREJELEO ........ 80

## SHUKRANI

Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na hekima katika safari hii ndefu ya kutafuta elimu ya juu. Pili, ninawashukuru kwa njia ya pekee wasimamizi wangu yaani Dkt. Nyachae Michira na Dkt. Prisca Jerono kwa mawaidha mengi waliyoyatoa kwa ukarimu mkubwa ili kunipa mwongozo bora wakati wote wa kuandika tasnifu hii. Ningependa kuwashukuru kwa njia ya pekee Dkt. Iribe Mwangi na Dkt. Evans Mbuthia kwa usimamizi wao wa masomo haya ya masafa ya mbali ili kuhakikisha kwamba tumeyakamilisha bila pingamizi nyingi. Sitawasahau wahadhiri wote walionifunza yaani Dkt. Jefwa, Dkt. Zaja, Dkt. Kineene wa Mutiso, Bw. Mungania, Dkt. Swaleh, Dkt. Mbatiah na Prof. Habwe. Ningependa pia kuzitoa shukrani zangu za dhati kwa Pasta Josephat Attaro kwa maombi yake pamoja na waombezi wenzangu. Mwisho kabisa ninawashukuru wasomi wenzangu kutokana na ushirikiano wa kutiana moyo wakati mgumu wa masomo yetu.

## MUHTASARI

Utafiti huu umeshughulikia uhakiki wa hali ya vijana katika *Vipanya vya Maabara* kwa kuegemea maudhui na wahusika. Katika sura ya kwanza, tumeangazia Somo la Utafiti, Madhumuni, Nadharia Tete, Sababu za kuichagua mada hii, Yaliyoandikwa kuhusu mada yenyewe, Msingi wa kinadharia pamoja na njia za utafiti. Sehemu hii kwa hakika ni kama msingi wa kazi yetu ya utafiti tulioufanya.

Katika sura ya pili tumejadili dhana ya uhusika kwa jumla. Tumeangalia aina mbali mbali za wahusika kama wanavyoainishwa na wataalam mbali mbali huku tukibainisha mwiingiliano mkubwa uliopo baina ya makundi hayo tofauti tofauti. Sura yenyewe ina umuhimu mkubwa katika kuwaelewa wahusika pamoja na usawiri na umuhimu wao katika kazi ya fasihi.

Sura ya tatu imeshughulikia wahusika. Katika sehemu hii, tumewachambua wahusika kwa kuangazia aina zao, usawiri wao pamoja na umuhuimu wao. Sifa zao mbali mbali vile vile zimejadiliwa. Hata hivyo umuhimu mkubwa zaidi umepewa vijana kwa kuonyesha jinsi gani wanavyotumiwa kama vipanya vya maabara pamoja na matatizo mbali mbali zinzowakumba.

Sura ya nne imeshughulikia maudhui huku uzito ukipewa matatizo yanayowakumba vijana katika sehemu za mijini nchini Kenya ingawa mji wa Nairobi umetumiwa kama mandhari ya riwaya hiyo. Mbali na matatizo, kunao vile vile ujumbe chanya ambao umeangaziwa kuwahusu vijana. Kwa vile vijana hawawezi kupatikana katika jamii isyo na wazee, kundi hili la watu wakomavu pia limehusishwa katika maudhui kwa sababu matatizo mengi yanayowakumba vijana yanasababishwa ama na wazazi au watu wengine wazima wenye ushawishi mkubwa katika jamii. Sura ya tano imebeba hitimisho la utafiti wetu kwa lengo la kudhibitisha ufanisi kwa utafiti wenyewe kwa mujibu wa madhumini na nadharia tete zetu. Tumebainisha matokeo ya utafiti pamoja na matatizo yaliyotukabili wakati wa kufanya utafiti huu. Hatimaye tumetoa mapendekezo kuhusu utafiti unaoweza kufanywa baadaye kuhusiana na kazi kama hii.

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Maana ya dhana ya kijana inatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Umoja wa Kimataifa unawatambulisha vijana kama mabarobaro wa jinsia zote ambao umri wao ni baina ya miaka ya kumi na mitano hadi ya ishirini na nne; kwa mujibu wa Ripoti ya Kimataifa kuhusu vijana 2011. Kulingana na sera ya kitaifa kuhusu vijana nchini Kenya, kijana ni mtu yeyote ambaye umri wake ni baina ya miaka kumi na mitano na thelathini. Haya ni kutokana na Tarakimu za Wizara ya Vijana na Michezo iliyobuniwa mwaka wa 2008. Kwa misingi hii na kwa kuzingatia sensa ya mwaka 2009, zaidi ya asilimia sabini ya watu wote nchini Kenya ni vijana.

Majukumu ya vijana katika jamii yamekuwa yakibadilika jinsi hali ya jamii inavyobadilika vilevile. Kwa mfano, katika mfumo wa maisha ya kiasili ya mwafrika kabla ya majilio ya wageni na elimu ya kimagharibi, malezi ya vijana pamoja na kuwaelekeza katika jamii yalikuwa ni wajibu wa jamii nzima. Hi ni kwa sababu watoto walikuwa ni mali ya jamii. Tabia potofu miongoni mwa vijana zilishutumiwa na watu wote kwa vile maisha yalikuwa ni ubia au ushirika. Watoto walikuwa chini ya jicho pekuzi la jamii kila wakati. Majukumu ya vijana vivyo hivyo yalikuwa bayana huku vijana wa kiume wakiandamana na wazazi wao wa kiume waliowafunza shughuli za kiume kama vile uwindaji na jinsi ya kuihami jamii hata kuikidhia familia yake mahitaji akishaoa. Wasichana nao walifundishwa mambo ya unyago yaliyozingatia utekelezaji kamilifu wa majukumu yao wakishaolewa. Katika hali hii ya maisha ya kitamaduni, vijana hawakuwa na changamoto nyingi kwa sababu kulikuwa na utaratibu wa kuwaelekeza kulingana na kila jamii.

Mfumo huu wa kiasili ambao ulijikita katika taratibu za tamaduni maalum ulivurugwa na majilio ya wakoloni pamoja na wageni wengine kutoka nchi za Kimagharibi. Mtagusano wa wageni hawa ulivuruga utaratibu wa mifumo ya ulezi ambayo ilikuwako. Elimu ya

kimagharibi ilileta mambo mapya na hata kuvuruga thamani pamoja na maadili katika jamii. Kwa mfano, vijana walilazimika kwenda shuleni na vilevile wazazi wao kutafuta kazi katika sehemu za miji ili kukidhi mahitaji mapya yaliyotokana na njia hizi mpya za maisha. Jinsi jamii zetu zilivyoegemea zaidi kuelekea utaratibu wa maisha ya kimagharibi ndivyo asasi zilizohusika moja kwa moja na malezi ya vijana katika jamii zilivyoendelea kuporomoka na hivyo kuwaacha vijana bila mwelekeo maalum wa kuwafunza maadili.

Jamii ya kesho inategemea vijana ambao ndio msingi wake. Iwapo basi msingi huo ni dhalili na unakosa uthabiti, basi taifa nalo linakosa matumaini. Baada ya uhuru kupatikana viongozi walioshika hatamu hawakuweka chini sera kabambe kuweza kushughulikia hususan maisha ya vijana. Hata waandishi wa kifasihi katika maandishi yao ya hapo nyuma hawakuwachukulia vijana kwa dhati sana katika uandishi huo ambapo majukumu yao ya uhusika hayakuwa muhimu sana. Nchini Kenya, waandishi wasomi wengi wao wakiwa wahadhiri katika vyuo vikuu vyetu ndio wamechukua jukumu la kuangazia maswala ya vijana. Haya yamedhihirika katika riwaya kama vile *Siku Njema* (Walibora, 2000), *Tumaini* (Momanyi 2006) na hata tamthilia kama vile *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (Kithaka wa Mberia 2004) na *Pango* (*Wamitila* 2003).

Hata hivyo riwaya ya *Vipanya vya Maabara,* (Mbatiah 2007) inajitokeza kama kazi ambayo imeangazia kabisa matatizo yanayowakumba vijana katika jamii na hata mchango mkubwa ambao vijana wanaweza kutoa kusuluhisha baadhi ya matatizo kama ukabila. Ingawa mazingira ambayo yamechukuliwa kama mandhari ni ya jiji la Nairobi na viunga vyake, matatizo na changamoto ambazo zinawakumba vijana hata kama Bob Kerogo, Wairi, Swaleh na hata Muli ni hakikisho nzuri sana la hali ya vijana katika taifa letu kwa jumla. Mbatiah kwa namna ambayo haijaelezwa wazi wazi hapo awali anatufanya kuona ni kwa nini vijana wanakumbwa na matatizo chungu nzima. Muli anabobea madawa ya kulevya kwa ajili ya

kukosa baba mzazi wa kumwelekeza. Bob na Freda wanasoma kwa taabu sana kwa sababu ya ulevi wa baba yao anayekata tamaa kwa sababu ya kutopandishwa cheo kazini. Wairi anakosa mwelekeo kwa sababu wazazi wake hawana nafasi ya kumwelekeza. Muda wao mwingi wamo katika harakati za kutafuta pesa. Hata mfumo wa elimu unachangia matatizo yanayowakumba vijana. Jamila kwa mfano anaenda chuo kikuu cha Egerton kusomea shahada ya B.Sc. ilhali roho yake ilitamani uhandisi. Riwaya hii imebeba uhalisia kamili kwa sababu imeandikwa katika nafsi ya kwanza ambayo inatunafanya kuhisi uyakinifu wa matukio yote. Kwa mfano: "Kweli bahati ni upepo. Tukio la kukutana kwangu na Vera lilipeperushwa na upepo hadi mikononi mwangu….." (uk 1).

### 1.1. Tatizo la Utafiti

Vijana wanachukua sehemu muhimu sana katika jamii yoyote ile. Mchango wao hauwezi kupuuzwa. Wao ndio msingi na tegemeo la taifa husika kwa siku zijazo. Kwa hivyo uthabiti wa kundi hili ni wenye umuhimu mkubwa kwa sababu athari zozote hasi kwalo huweza kuleta matokeo mabaya katika jamii hiyo.

Nchini Kenya vijana ndio wanaochukua asilimia kubwa zaidi ya wananchi wote. Jambo la kusikitisha ni kwamba vijana hao wanaonekana kukumbwa na matatizo chungu nzima ambayo chanzo chake kinafaa kichunguzwe.

Hivyo basi tatizo la utafiti wetu ni kuchunguza ili kubainisha aina za changamoto zinazowakumba vijana nchini Kenya pamoja. Mbali na utambuzi huo wa changamoto hizo utafiti huu vilevile unalenga kutathmini msingi wa matatizo hayo. Tunanuiya kubainisha hasa ni nini kinachochangia matatizo haya ndipo suluhisho liweze kupatikana ili vijana wapate afueni maishani mwao.

Utafiti wenyewe utaangazia matatizo ya jumla yanayokumba vijana na vilevile yale yanayojitokeza katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara*.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

i. Kuzichunguza changamoto zinazowakumba vijana katika jamii.

ii. Kutathmini misingi na kiini cha matatizo yanayowakumba vijana katika jamii.

iii. Kubainisha umuhimu wa vijana katika ubomoaji wa ukabila.

## 1.3. Natharia Tete

i. Malezi duni ndicho kiini cha changamoto zinazowakumba vijana katika jamii ya sasa.

ii. Sera duni za serikali ndizo zinachangia pakubwa matatizo yanayowakumba vijana.

iii. Ubomoaji wa ukabila unawategemea vijana.

## 1.4. Sababu za Kuichagua Mada Hii

Sababu hasa iliyotufanya kuchagua maada hii ni kwamba inahusiana na kundi muhimu sana katika jamii ambalo ni la vijana. Umuhimu huu unatokana na sababu fulani. Kwanza wanawakilisha asilimia kubwa sana ya idadi ya watu wote nchini Kenya. Mbali na idadi yao kubwa, wanawakilisha uhai wa taifa. Katika uhai, tunamaanisha kwamba hali ya siku zijazo ya taifa inawategemea wao. Nchi yoyote ambayo haina kitengo cha kutegemea cha vijana bila shaka haina matumaini kwa siku zijazo. Haya yanatokana na ukweli kwamba vijana ndio viongozi wa kesho na vile vile msingi wa kizazi cha baadaye katika taifa. Nchi yoyote ambayo haina vijana ni sawa na family tasa ambayo haina matumaini yoyote ya kukiendeleza kizazi chake.

Sababu nyingine iliyotufanya kuichagua mada hii inahusiana na kutokuwepo kwa maadili miongoni mwa vijana. Kuna mambo mengi hasi yanayoshuhudiwa miongoni mwao. Mambo yenyewe ni anuwai na yanagusia ulevi, matumizi ya mihadarati, uzinzi na hata uhalifu. Katika msingi wa maisha ya kitamaduni, maadili yalisambazwa na kuhimizwa miongoni mwa vijana. Vijana hawakuruhusiwa kunywa pombe wakiwa chini ya umri fulani ilhali kupata mimba nje ya ndoa ulikuwa ni mwiko. Basi imekuwaje kwamba kiwango cha maadili

katika jamii kimezorota jinsi hii? Kwa nini vijana wajihusishe na uhalifu? Katika *Vipanya Vya Maabara*, kuna matukio ambayo yanatokana moja kwa moja na kuzorota kwa maadili. Vijana kama Bob, Wairi, Jamila na hata Gaceri wanashiriki katika vitendo vya ngono kutokana na athari za kijamii na misukumo ya mahirimu. Mbali na misukumo hii, ukosefu wa malezi bora unachangia pakubwa. Mbona Swaleh ambaye babake ni polisi mwenye jukumu la kukabiliana na uhalifu awe ni jambazi? Hiki ni kinaya kwamba mwana wa inspekta wa polisi amekuwa ni jambazi sugu. Ingawa changamoto zinazowakabili vijana ndizo zinazochukua sehemu kubwa ya usawiri wao, hiyo si sababu pekee iliyotufanya tuichague mada hii.

Vilevile katika kuichagua mada hii tulivutiwa na hali hii ya vijana kutumiwa kama *Vipanya Vya Maabara.* Ni katika misingi gani hasa ambapo vijana wametumiwa kama *Vipanya au v*inyama vya kufanyiwa majaribio? Sehemu moja ambayo imetiliwa uzito katika hali hii ya kufanyiwa majaribio ni mfumo wa elimu wa 8-4-4 ambao ulianzishwa bila kufanyiwa majaribio ya kukadiria ufaafu wake. Ulianzishwa kwa lengo la kuwapa wasomi stadi za kuwawezesha kujitegemea lakini hakuna karakana zilizojengwa wala vifaa kununuliwa katika shule ili kuwezesha mtaala kushughulikiwa ipasavyo. Mfumo wenyewe ulisukumwa na misimamo ya kisiasa. Hatimaye kukawa na wasomi wengi wasiokuwa na ujuzi wa kuwawezesha kujitegemea. Hivyo basi kwa misingi ya yale ambayo tumeeleza, tulishawishika kuichagua mada hii ili tuifanyie utafiti.

**1.5. Upeo na Mipaka**

Utafiti huu unahusu uhakiki wa vijana katika *Vipanya Vya Maabara.* Utafiti wenyewe unatilia maanani matatizo yanayowakumba vijana kwa jumla pamoja na yale yanayoibuka katika riwaya. Wahusika na maudhui ni sehemu nyingine inayoshughulikiwa. Sehemu hizi zinaangaziwa kwa sababu zinachangia pakubwa kuelewa hali ya vijana na hivyo kufanikisha

uhakiki wa hali hiyo. Katika maudhui tunapata ujumbe pamoja na mafunzo ambayo yamefungamana na hali ya vijana kwa jumla.

## 1.6. Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili

Katika sehemu hii tumeangalia yaliyoandikwa kuhusiana na yale tunayoyashughulikia. Ingawa hatukuweza kuona kazi ambayo hususan inashughulikia riwaya ya *Vipanya vya Maabara* moja kwa moja, tumepitia kazi kadhaa ambazo zinashughulikia maswala ya vijana na ambazo zimekuwa ni za msaada mkubwa sana kwetu. Mwandishi mmoja ambaye kazi yake imemulika maswala ya vijana ni Kezilahabi katika riwaya ya *Kichwa maji* (1974). Nkonge (2006) ameangazia athari za udhanaishi katika riwaya za *Kichwa Maji* (1974) na *Nguvu ya Sala* (Wamitila 1999). Baadhi ya mambo ambayo ameshughulikia kuhusu vijana ni kama vile mapenzi na ndoa, maisha na kifo, malezi, uozo wa jamii na dini. Maswala haya yanaoana na baadhi ya yale ambayo tunayashughulikia katika utafiti huu kwa hivyo kazi yake imekuwa ni ya manufaa makubwa kwetu. Tofauti ni kwamba huku akitumia nadharia ya udhanaishi sisi tumetumia nadharia ya uhalisia.

Lugano (1989) vile vile ameangalia namna Kezilahabi amewachora wahusika wake wa kike na ikikumbukwa kwamba Kezilahabi ameangazia zaidi wahusika vijana kama vile Kazimoto *Kichwa Maji* (1974) na *Rosa Mistika* (1971). Kazi hii imetupa msaada mkubwa.
Hata hivyo, badala ya kuwashughulikia tu wahusika wa kike, sisi katika tasnifu hii tunaangazia vijana kwa jumla bila kuegemea jinsia moja. Katika kufanya hivyo tunawasilisha picha inayoonyesha hali halisi ambayo inahusiana na matatizo yanayowakumba vijana, wawe wa kike au wa kiume Mutua (2007) ameangazia *Mitazamo ya Vijana na Wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili*. Kilichotulekeza kupitia kazi hiyo ni mitazamo ya vijana katika ukombozi wa wanawake. Hata hivyo tulionelea kwamba mkabala wake huo ulikuwa umejikita katika ukombozi wa wanawake pekee. Katika utafiti

wetu kuhusu uhakiki wa hali ya vijana katika *Vipanya vya Maabara*, tulihisi kwamba ukombozi ambao vijana wanahitaji uwe ni wa malezi, ajira au elimu unafaa kushughulikia vijana wote bila kujali jinsia zao.

Kiango (1992) ameangazia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Amesema kwamba mwanamke amewasawiri kama mtu asiye na usawa na mwanamume na kuchorwa kama kitega uchumi, mzinifu, mtoaji mimba na mtupaji watoto. Utafiti wake umetufaa kwa kuangazia swala la wanyonge. Utafiti wetu unapiga hatua zaidi na kuonyesha kuwa wanyonge si wanawake tu bali vijana pia ambao hudhulumiwa na makundi mbalimbali katika jamii kama vile walimu, wazazi, mawaziri na watu wengine wenye uwezo katika jamii. Mogambi (1983) anahakiki *hali ya wanyonge kama wanavyojitokeza katika riwaya tatu za S. Mohamed.* Uhusiano wa kazi hii na yetu ni kwamba tumewachukulia vijana kama kundi ambalo linadhalilishwa na jamii katika *Vipanya vya Maabara*. Anapodhihirisha mambo yale ambayo yanachangia unyonge wao, anatusaidia kuelewa masuluhisho ambayo yanahitajika ili kukabiliana na kuondoa unyonge huu.

Katola (2006) alishughulikia swala la udhalimu dhidi ya wahusika wa kike kama unavyojitokeza katika kazi za waandishi wa jinsia zote mbili katika tamthilia za Kiswahili. Ingawa amelenga tu wahusika wa kike, sisi katika tasnifu yetu tunaangazia dhuluma ambazo vijana wanatendewa katika jamii bila kuegemea jinsia moja. Basi pengo hilo la kutoangaziwa kwa matatizo yanayowakabili vijana kwa jumla bila upendeleo au kuutilia uzito jinsia moja ndilo lile ambalo utafiti huu unanuia kuziba.

**1.7. Msingi wa Kinadharia**

Msingi wa kinadharia ambao tumeutumia katika tasnifu hii ni wa uhalisia. Wafula na Njogu (2007) wanaelezea uhalisia kama nadharia muhimu zaidi ya uandishi kuwahi kuzuka katika

karne ya kumi na tisa na ishirini. Uhalisia huenda ukaendelea kuathiri ulimwengu hata katika karne ya ishirini na moja. Chanzo cha uhalisia ni maeneo ya Ulaya katika karne ya kumi na tisa ambapo mapinduzi ya kiviwanda yalizusha mambo mapya kama vile kuzuka kwa miji, makabwela pamoja na matatizo ya maisha yaliyotokana na upanuzi wa miji hiyo. Shida hizi ziliwafanya wanasanaa waandishi kuanza kukejeli na kuupuza ulimbwende uliokuwa ukithaminiwa enzi hizo na watunzi ambao matamanio yao yalikuwa ni ya kinjozi tu yakilinganishwa na shida zilizowakabili watu katika mazingira hayo. Yaani walimbwende walitunga na kuandika fasihi kuhusu mambo ya kindoto.

Ingawa uhalisia kama tapo la kuwaelekeza watunzi ulianza kudhihirika kuanzia mwaka wa 1800 nyakati za mwandishi wa kifaransa Gustav Flaubert, dhana ya uhalisia ilianza kujitokeza zamani sana katika kipindi cha enzi za kati, yaani baina ya 1100-1500 baada ya Kristo. Ilipitia mabadiliko mengi ya kimatumizi na wataalam kama vile Emmanuel Kant (1790) na hata Schiller (1798). Ili kuelewa ufaafu wa uhalisia kama msingi wa kinadharia wa tasnifu hii tumeangazia maelezo ya wataalamu wengine. Mbatiah (2001) anarejelea uhalisia kama istilahi inayorejelea kimsingi mtindo wa uandishi unaojishughulisha na utoaji wa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi. Anaendelea kusema kwamba mkondo huu wa uandishi unahusiana zaidi na riwaya. Mbali na hayo, uhalisia vilevile unaelezwa kama tapo mahususi la uandishi ambalo lilizuka katika maeneo ya Ulaya katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa na kusambaa katika maeneo mengine ya ulimwengu. Wasanii walioshughulikia tapo hili waliamini kwamba ukweli uliweza kupatikana katika maisha pamoja na shughuli za kawaida za kila siku za binadamu akiwa katika mazingira yake halisi ya kijamii. Mazingira kama hayo ni lazima yasawiriwe jinsi yalivyo na bila kutiliwa chumvi.

Baadhi ya waandishi wa awali wa kipindi hiki ambao maandishi yao yalisisitiza hali ya ukweli walitoka nchini Ufaransa wakiwemo Balzac, Stendhal na Gustav Flaubert. Waandishi hawa wa kifaransa walichangia sana kuyawekea msingi maandishi yenye mwegemeo wa kihalisia. Akizungumzia nadharia hii, Wamitila (2003)) anasema kwamba uhalisia una historia ndefu sana na ulizuka kama vuguvugu la kupinga mtazamo wa ulimbwende. Anakubaliana naye Mbatiah kwamba uhalisia, kama mkondo wa uandishi, unasisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi, kama yalivyo kila siku. Anadai kwamba George Lucas, mfuasi wa Karl Marx kutoka Hungary ni mmoja wa wataalamu wanaohusishwa na nadharia hii na ambao mchango wao umekuwa na athari kubwa sana katika tapo hili. Lucas aliamini kwamba uhalisia ulifaa kusawiriwa katika ukamilifu wake na vilevile picha ya uhalisia inayoshughulikiwa ni lazima ichunguzwe kwa undani ili kuzielewa sheria za mabadiliko ambazo husababisha hali ya uhalisia kwa wakati fulani. Kwa msingi huu, Lucas aliamini kwamba mwanasanaa au mwandishi ni lazima aelewe kwamba ulimwengu huu anamoishi ni changamano na hubadilikabadilika. Kwa hivyo, mwandishi au mwanasanaa huyo hana budi vilevile kuvielewa vipengele vya kijamii ambavyo vinasababisha mabadiliko kama hayo na kuathiri hali ya uhalisia kila wakati. Wanaoegemea katika tapo hili wanaamini kwamba yale yanayoshughulikiwa katika maandishi fulani ni lazima yaweze kuthibitika katika ulimwengu halisi.

Mbali na wataalamu waliotajwa awali kama vile Lucas na Flaubert, mwanafalsafa mwingine ambaye anachukuliwa kama mhimili wa nadharia hii ya uhalisia ni Hegel ambaye katika kitabu chake maarufu cha Aesthetik (ujumi) anatumia neno uhalisia kuelezea kazi ya fasihi ambayo inawakilisha ulimwengu au jamii ambamo wanahusika waliomo wanatenda mambo kulingana na wanavyochochewa na hali iliyomo (Wamitila 2003). Msokile, (1993) analielezea tapo la uhalisia kama mtindo wa sanaa wa kuonyesha maisha kama yalivyo na kwamba mambo yaliyotokea katika ulimbwende ndiyo yaliyosababisha kuzuka kwa uhalisia.

Baadhi ya kauli za kimsingi kulingana na Wamitila na ambazo ni muhimu kuhusu nadharia ya uhalisia ni kwamba inajikita katika ushabihikweli. Maana yake ni kwamba kazi yoyote inayoandikwa katika msingi huu ni sharti ikaribiane na kuelezea ukweli katika jamii husika. Kwa hivyo maandishi yoyote yanayoegemea katika uhalisia huchukuliwa kwamba yote yaliyomo yanaoana na kuwiana na ukweli katika jamii wanayoiangazia. Uhalisia vilevile haujatuama mahali pamoja tu. Yaani usawiri na uelewa wa uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine na kwamba kila kizazi kina uhalisia wake. Kile ambacho kizazi kimoja kinachukulia kama uhalisia kinaweza kikawa tofauti kwa kizazi kingine. Wasanii wanaoandika katika misingi ya uhalisia ni sharti waelezee ukweli na ukweli huo uelezwe kwa maneno halisi. Sanaa vilevile inafaa kuwa aminifu na iseme ukweli kwa kuonyesha hali halisi ya mazingira. Katika uhalisia basi sanaa ilichukuliwa kama kioo cha jamii. Kwa hivyo tumeichukua nadharia hii ya uhalisia kama msingi wa uhakiki wetu kwa sababu ya maswala ambayo yameangaziwa katika *Vipanya Vya Maabara.*

Maswala haya si ya kidhahania bali yanaonyesha hali halisi na ukweli wa matatizo yanayowakumba vijana katika jamii. Huu ndio uhalisia ambao tulichukua kama msingi wa kinadharia wa tasnifu yetu . Riwaya ya *Vipanya vya Maabara* bila shaka inaoana na nadharia hii kwa sababu shida zile zinazowakumba vijana ni kiwakilishi kamili cha hali halisi ya jamii tunamoishi. Baadhi ya matatizo yanayowakumba vijana katika riwaya hii kama vile uhusiano wa kimapenzi baina ya wanafunzi na walimu wao, ukosefu wa ajira, madawa ya kulevya, ubakaji, athari za ukimwi, uhalifu na kadhalika ni maswala halisi na nyeti katika jamii ya sasa. Hata hivyo katika sehemu hii inafaa kutaja tu kwamba kuna aina kadhaa za uhalisia ingawa hatutauhusisha na kazi hii yaani uhalisia hakiki, uhalisia nafsi, uhalisia ajabu na uhalisia wa Kisosholisti au kijamaa.

## 1.8. Njia za Utafiti

Kimsingi, utafiti wetu ulikuwa ni wa maktabani ili kurejelea makala mbali mbali yanayolenga maswala ya vijana. Kwanza kabisa tuliisoma kwa kina *Vipanya vya Maabara*. Mbali na riwaya hiyo tulizisoma riwaya zingine ambazo zinaangazia changamoto za vijana. Marejeo mengine yaliyokuwa muhimu katika utafiti huu ni tasnifu za wasomi wengine na ambazo zilikuwa na uhusiano fulani na utafiti wetu hasa zile za maswala ya vijana. Vilevile tulisoma majarida ambayo yanashughulikia maswala ya vijana. Matumizi ya mtandao kutafuta habari mwafaka kuhusu vijana na zinazohusiana na utafiti huu vilevile yalikuwa ya msaada mkubwa.

## SURA YA PILI

## UHUSIKA

### 2.0 Utangulizi

Tatizo letu la utafiti kama tulivyosema katika sura ya kwanza ni uhakiki wa hali ya vijana katika *Vipanya vya Maabara,* hasa kwa kuangazia wahusika na maudhui. Kwa vile vijana ndio wahusika ambao wamechukua sehemu kubwa ya riwaya hii ilitubidi tuangazie kwanza swala pana la uhusika na wahusika ili uwe ndio msingi wetu wa kuhakiki vijana na namna ambavyo wamesawiriwa au kuwasilishwa katika riwaya nzima. Kwa hivyo katika sura hii tulijadili kwa kirefu dhana ya uhusika pamoja na makundi mbalimbali ya uainishaji wa wahusika. Isitoshe tuliyahakiki makundi yenyewe ili kubaini ufaafu wake na pale ilipowezekana tulipendekeza makundi zaidi ya uainishaji.

### 2.1. Dhana ya Uhusika

Kuna wataalamu wengi ambao wamewahi kulizungumzia swala la uhusika. Katika *Kamusi ya Fasihi* (Mbatiah: 2001), Mbatiah anaelezea uhusika kama utaratibu wa kuwaumba wahusika pamoja na kunga zinazokwenda na utaratibu huo, hasa utofautishaji na ukuzaji wao. Tunaangalia dhana hizi kwa msingi kwamba wahusika ni viumbe ambao huumbwa, huhuishwa na kukuzwa na msanii. Uumbaji huu ni jambo linaloambatana na ubunifu mkubwa. Mbatiah anaendelea kusema kwamba mtunzi anaweza kutumia dailojia ambapo tabia za wahusika hubainika kutokana na msanii au mazungumzo yao. Tunaafikiana na Mbatiah katika jambo hili kwa sababu mtu mhalifu anapozungumza maelezo yake hubainika kutokana na mazungumzo yake na vilevile mazungumzo ya mtu mkarimu yatadhihirisha tabia hiyo.

Mbinu nyingine ambayo mwandishi atatumia ili kufafanua hulka ya mhusika fulani ni kwa kutoa maelezo kumhusu mhusika lengwa. Sisi kama wasomaji itatubidi tuamini yale ambayo

mwandishi anasema ingawa tuna uhuru wa kutoa maoni yetu, ikiwa usawiri ambao mhusika fulani amepewa hauna uhalisi kulingana na yale ambayo tunayajua kuhusiana na mhusika wa aina hiyo akiwa katika mazingira fulani tuliyo na uelewa nayo. Watunzi wengine hata hivyo watachanganya mbinu zote mbili za kuwaumba wahusika yaani kwa kuwahuisha na kuwapa nafasi ya kuzungumza. Tungependa kuongezea kwamba mbali na maelezo kumhusu mhusika au nafasi anayopewa ya kuzungumza, mhusika pia huumbwa kupitia kwa matendo yake.

Wamitila (2003:278) anaelezea uhusika kama mbinu na mikakakati inayotumiwa na mwandishi ili kuwasawiri wahusika katika kazi yake. Waandishi wote wanaonuia kupata ufanisi katika kazi yao ya kubuni ni lazima watilie maanani swala la uhusika kwa sababu mhusika ndiye uhai wa kazi fulani. Matukio katika kazi fulani ni lazima yaafikiane na wahusika. Kwa mfano katika *Vipanya vya Maabara*, ni jambo la kawaida kwa kijana Bob Kerogo ambaye asili yake ni Meru kuwa na uraibu wa kutafuna miraa ambapo haihalisi mhusika kama Padre Giovani kuwa na tabia kama hizo kwani huduma yake kama kasisi inahitaji kiwango fulani cha uadilifu na utakatifu.

Wamitila anasema kwamba kuna mbinu kadhaa za kuwaumba wahusika. Moja wapo ya mbinu hizo ni ile anaayoita mbinu ya kimuhtasari ambapo mwandishi anaweza kutoa wasifu wa mhusika kiumbo na matendo. Hufanya hivi kimaelezo yeye mwenyewe kama mwandishi ama anaweza kumtumia mhusika fulani kutoa wasifu kuhusu mhusika mwenzake. Kwa mfano katika uk 36, Bob anatoa maelezo kuhusu umbo lake Wairi na namna alivyokuwa mrembo. Mbinu hii inafanana na ile ambayo Mbatiah aliita ya maelezo na hufaa sana wakati tunapotumia mbinu rejeshi kutoa wasifu wa marehemu ambaye hatuna uwezo wa kumhuisha ili aweze kutenda tena na kuzungumza.

Katika kuwaumba wahusika, Wamitila ametaja mbinu nyingine ya kuwaumba kwa kuwashirikisha katika matendo na mazungumzo ambapo katika mazungumzo na matendo

hayo, tunapata kuzielewa hulka zao. Kwa hakika hii ndiyo mbinu yenye uhalisia zaidi kwani hakuna mtu ambaye huzungumza tu daima katika mawasiliano yake pasi na kutenda au atende tu bila kunena. Hata bubu huhusisha sana lugha ya ishara na vitendo katika mawasiliano yake. Tunachosema hapa ni kwamba vitendo vilevile hutupa wasifu wake mtu au uhusika wake mtu ambapo mbinu ya aina hii ya kumbuni mhusika inaweza kuitwa mbinu ya kidrama au utendaji. Katika *Vipanya vya Maabara* (uk 67) katika sehemu hii mwanamke yule mzungu, Vera, akiwa na Bob ukingoni mwa Ziwa Manyara alizivua nguo zake zote na kubaki na chupi. Tendo hili linamsawiri kama mtovu wa maadili.

Wahusika vilevile; kulingana na Wamitila wanaweza kuumbwa kwa kutumia mbinu ya kisaikolojia ambayo inahusishwa na mazungumzo nafsia. Aghalabu, mtu akiwa katika hali ya kutafakari au kukumbwa na matatizo mengi, huweza kuwaza kwa sauti kwa kujisemeza mwenyewe na tukapata hulka yake. Kwa mfano katika *Vipanya vya Maabara* uk 80, Bob alimpeleka Vera kwake nyumbani Karen ambapo alipomkaribisha kwa chakula cha maini, katika fikira zake, Bob alijisemeza kimoyomoyo "Laiti kungekuwa na ugali!" Hapa tunapata sifa ya mtu anayependa sima iandamane na kitoweo au labda wengine wamhakiki kama kijana asiyestaraabika.

Matumizi ya majazi au majina ambayo yanashabihiana na sifa za mhusika fulani vilevile imeelezwa naye Wamitila kama mbinu ya kumwumba mhusika. Tunalotaka kusema hapa ni kwamba ukimpa mhusika jina la kimajazi basi unawajibika kuhakikisha kwamba unamhusisha mhusika huyo ili atende vitendo au aseme mambo ambayo yanaonyesha uhalisia wa jina ulilompa. Wamitila (2002:2-6-27) amependekeza mbinu ya ulinganuzi na usambamba ambapo mhusika fulani ambaye tabia yake ni kinyume kabisa na tabia za yule mwingine waliye na ujirani. Naye huweza kuchangia kubainisha tabia za huyo mwingine au "ulinganisho" namna alivyourejelea. Tungependa kudai kwamba Mbaabu, mjombake Bob, na

mkewe katika *Vipanya Vya Maabara* wanatosheleza maelezo haya kwani huku Mbaabu akiwa mkarimu sana, mkewe alikuwa ni kinyume kabisa, yaani mtu bahili.

Katika sehemu hii, kile ambacho tunatilia umuhimu ni usawiri wa mhusika fulani. Iwapo huelewi msingi wa uhusika basi haitakuwa rahisi kwako kama mtunzi kuwaumba na kuwasawiri wahusika wako ipasavyo. Vivyo hivyo kwa wahakiki kama sisi ambao lengo letu katika tasnifu hii ni kushugulikia uhakiki wa hali ya vijana katika *Vipanya vya Maabara* ni muhimu kwetu kulielewa na kulieleza swala hili la uhusika ambalo linatuelekeza katika sehemu nyingine muhimu inayofuata katika sura hii; yaani uainishaji wa wahusika katika fasihi kwa jumla. La msingi kuelezea hapo ni kwamba uhusika ni uti wa mgongo wa kazi yoyote ya fasihi hususani ya kubuni kwa sababu uwasilishaji wa maudhui itakikanavyo hutegemea aina ya wahusika ambao msanii amewabuni na iwapo wanachangia ukuaji wa maudhui kwa njia inayofaa na ya kuridhisha. Hii ni kusema kwamba uhusika huo ni sharti uwe na uyakinifu.

## 2.2. Uainishaji wa Wahusika

Uainishaji ni dhana inayotumiwa kurejelea hali ya kuvigawa vitu katika makundi ya ulinganifu kwa kutegemea vigezo au mikabala fulani. Ni kwa nini tushughulikie uanishaji wa wahusika? Uainishaji na uhakiki una uhusiano kwa sababu unapowahakiki wahusika unatumia vigezo fulani katika kuwajadili na ndipo uwaweke kisahihi katika makundi hayo tofautitofauti ya uhakiki. Lililo muhimu kudai hapa ni kwamba uanishaji si jambo rahisi kwa sababu huwa unategemea mkabala ambao mhakiki fulani anachukua katika uchanganuzi wake wa wahusika wale. Isitoshe makundi tofautitofauti yanayoibuka yanahusiana na hata kuingiliana kwa njia nyingi ambapo hakuna namna ambavyo kundi fulani linaweza kudai kujitosheleza na kujisimamia. Kwa kusema hivi tunamaanisha kwamba kundi fulani la uainishaji haliwezi kuwepo katika ombwe tupu, bali huwepo katika mtagusano na makundi

mengine. Katika sura hii tunawaainisha wahusika katika ujumla na upana wake bila kujikita hasa katika *Vipanya Vya Maabara* ili kuupa uhakiki mtazamo mpevu, lakini pale ambapo tunaamini kwamba aina hiyo ya wahusika wamepewa umuhimu katika riwaya hiyo basi tutasisitiza hilo tunaposhughulikia kundi hilo.

## 2.3. Aina za Wahusika

Njogu na Chimerah (2007) wametumia utaratibu wa kugawa ambao una ubia au sifa za kiulimwengu ambapo aghalabu kazi ya kifasihi yenye ubunifu huwa na wahusika wa aina hiyo na ni mgao ambao hata sisi katika tasnifu hii tunakubaliana nao na isitoshe tunaamini kwamba katika *Vipanya Vya Maabara* , uainishaji huu una mashiko.

## 2.4. Wahusika Wakuu

Kama jina linavyoelezea, hawa ndio viumbe wanaobuniwa na mtunzi ili wawe ni nguzo ya kazi yao. Wanakuwa ni kama msingi ya kazi hiyo ambapo dhamira kuu pamoja na maudhui mengine muhimu hudhihirika zaidi kupitia vitendo vya wahusika wa aina hiyo. Msuko wa hadithi aghalabu huwa unaelekezwa na wahusika wao hao ambao ndio uhai wa kazi fulani na kama inavyodaiwa na wataalamu wengi, wao ndio moyo wa hadithi fulani, wakiondolewa ghafla basi hadithi hiyo itakoma. Kwa kweli ni muhali sana kuwa na hadithi ambayo haina mhusika mkuu. Lililo muhimu ni kwamba hili ndilo kundi lenye ubia na ambalo linaweza kudai haki ya kuwa katika riwaya zote. Huu ukuu wa mhusika huwa unajengeka katika msingi fulani. Ili kuthibitisha mwingiliano uliopo baina ya makundi tofauti ya uanishaji tumetaja na kueleza makundi mengine ambayo yanaingiliana sawa na wahusika wakuu.

Aghalabu wahusika wakuu huwa ni wa miraba minne yaani wana sifa changamano ambazo zinakaribiana sana na za binadamu wa kawaida. Wanaweza kutumiwa kuelezea uovu au wema. Ikiwa mwaandishi ananuia kumfanya mtu mwema awe ndiye nguli wa hadithi

anayewakilisha maslahi au matakwa ya wengi katika jamii, basi sifa za wema ndizo zitakuwa na umuhimu au za kubainika zaidi. Sifa zile mbaya zinazowakilisha uhalisia wa binadamu vilevile zitajitokeza. Ikiwa huyu mhusika mkuu ndiye nduli au hasidi wa yule nguli basi uovu wake utapewa umuhimu zaidi kuliko wema ndipo uhasidi ule uonekane. Katika *Vipanya Vya Maabara,* Bob ndiye mhusika mkuu na akiwa katika nafasi hiyo, mtunzi anamfanya atende mabaya mengi ambayo ni kawaida kwa kijana wa umri wake kutenda. Baadhi ya matendo haya ni kama vile kushiriki katika starehe. Ingawa si lazima kwa vijana wote kujihusisha katika mambo ya mapenzi wengine wao hushiriki ngono bila hathari yoyote hasa kwa kuwa na zaidi ya mpenzi mmoja.

Katika uhakiki huu wa mhusika mkuu tungependa pia kusema kwamba ni wahusika wa aina hii ambao huwa ni wakwenza au wakwezwa yaani wale ambao wameinuliwa juu kiuadilifu au kimsimamo kuliko wahusika wa kawaida. Shaaban Robert katika maandishi yake alikuwa na wahusika kama hawa. Katika *Kusadikika* (1957) tulikuwa na Karama na hata wale wajumbe sita waliozuru maeneo sita ya dunia kwa lengo la kuleta habari mpya na zenye manufaa kwa taifa la Kusadikika lakini wakapuuzwa. Vilevile katika *Kifo Kismani* (Kithaka wa Mberia, 2001) kijana Mwelusi ni mhusika mkwezwa kwa sababu amepewa umaarufu wa kumwezesha kumtatiza mhusika kiongozi shupavu kama Mtemi Bokono. Katika *Vipanya Vya Maabara* huenda tusiwe na mifano kama hiyo. Kwa hivyo ni jukumu lake mwanasanaa mwandishi mbunifu kumsawiri mhusika wake mkuu katika hali ambayo haiachi tashwishi yoyote kuhusu ni nani ambaye ndiye mhusika mkuu.

### 2.5. Wahusika wasaidizi au wajenzi

Kwa hakika, wahusika wakuu hawezi kujijenga mwenyewe na wala hawawezi kushirikiana na nafsi zao katika utendaji kazi wake. Katika uhakiki huu wa wahusika tunalodai ni kwamba kundi lingine la uhusika ambalo ni lazima liwe katika kazi ya riwaya ni hili la wahusika

wasaidizi au wajenzi. Wema au ubaya wa mhusika mkuu unadhihirika kupitia uhusiano wake na wahusika wengine. Hii ina maana kwamba licha ya dhana ya wahusika wasaidizi kuweza kuibua hisia kuwa wahusika wa aina hii si muhimu sana jinsi walivyo wahusika wakuu, hayo si kweli kwa sababu bila hawa basi wahusika wale wakuu huenda wakawa ni "ganda tupu" bila msukumo wowote wa kuwafanya waaminike katika matendo pamoja na mazungumzo.

Mwandishi wa *Vipanya Vya Maabara* katika msuko wa hadithi yamkini alikuwa amepanga jinsi maisha yake Bob yangebadilika kutoka hali ya umaskini kama kijana wa kuosha magari hadi kuwa tajiri ambaye alimiliki mali na kuishi katika mtaa wa kifaari. Ili kuyapitia yote hayo na hatimaye kufikia kilele hicho cha maisha, ilikuwa ni muhimu awepo mhusika msaidizi au mjenzi wa kuchangia kufanyika kwa yote haya kwa sababu Bob mwenyewe hangeyasababisha matukio kama hayo kutendeka. Kwa kumpa Bob nafasi ya kumwendesha katika gari lake mara kwa mara, Vera alimfungulia mlango kwa sababu ni kutokana na mojawapo ya safari hizi katika Mbuga ya wanyama ya Ziwa Nakuru ambapo Bob alishuhudia kisa ambacho baadaye kiliyabadilisha kabisa maisha yake.

Mbali na kuchangia msukumo huo wa matukio, wahusika wajenzi vilevile wanasaidia sana katika ukamilishaji wa maudhui. Kwa mfano, tunapolizungumzia swala pana la matatizo ya malezi yanayowakumba vijana na tumwangazie Bob kama mmoja wa wahasiriwa, bila shaka babake Konstebo Kerogo anajitokeza kama mhusika muhimu kwa sababu kuingilia kwake ulevi wa kupindukia kunamfanya aache kuwajibika katika ulipaji wa karo ya wanawe na hivyo kuathiri pakubwa elimu yao na hata kuvuruga matokeo ya mitihani yao hatimaye. Kwa hivyo ingawa wahusika hawa wakitazamwa kijuujuu huenda wakapuziliwa mbali kama wasio muhimu, huchangia pakubwa sana katika kuelewa mwendo wa jamii fulani. Mwingiliano wao na mhusika mkuu hutuwezesha kumwelewa zaidi huyo mhusika mkuu. Katika hali yao ya ubinafsi, wahusika hawa wasaidizi wanaweza vilevile kuwa na sifa zinginezo za uhusika

kwa sababu hakuna vile mhusika atakuwa tu na aina moja ya sifa kwa sababu hiyo si hali ya kawaida.

### 2.6. Wahusika wa Miraba Minne na wa Mraba Mmoja.

Dhana hii ya miraba minne au mraba mmoja katika uanishaji wa wahusika inajitokeza tunapomhakiki mhusika kwa msingi wa sifa zake ambapo mhusika wa miraba minne huwa na sifa changamano, zingine chanya na zingine hasi. Kwa kweli tukizungumzia mhusika fulani ni nadra awe tu na aina moja ya sifa ama nzuri tu pekee au mbaya tu pekee. Lakini kwa vile katika maandishi mhusika huwa ni kiumbe chake mwandishi alichokibuni kwa madhumuni fulani huenda akamsawiri atakavyo, kutegemea lengo lake. Hivi ni kusema kwamba mhusika wa miraba minne ni yule ambaye anabainisha sifa changamano, zingine zikiwa nzuri na zingine mbaya. Kwa mfano Bob Kerogo katika *Vipanya vya Maabara* anabainika kama mhusika wa miraba minne. Tunapomhakiki kwa misingi ya tabia zake za kimapenzi tunamwona kama mhusika mzinifu sana mwenye tabia za ukware lakini licha ya udhaifu huo, vilevile anajitokeza kama kijana mwaminifu sana. Wakati aliposhuhudia waziri Rashid Hamisi akiuburuta mwili wa mwanamke, ambaye baadaye alikuja kubainika kama Rita King bintiye Seneta Humphrey King wa Marekani, aliweza kukiokota kipochi ambacho kilikuwa na hata fedha mle ndani lakini hakuchukua chochote.

Kwa upande mwingine mhusika wa mraba mmoja huwa na sifa moja ambayo imekuzwa zaidi. Tunaweza kudai kwamba katika *Vipanya vya Maabara,* wahusika kama Swaleh, Muli na Freda ni wa mraba mmoja kwa sababu wanadhihirisha aina moja tu ya sifa zao. Kwa mfano Swaleh na Muli wanahusishwa tu na sifa mbaya kama vile wizi wa kimabavu, matumizi na ulanguzi wa madawa ya kulevya na hata ubakaji kwa upande wa Muli. Uhalifu huo ndio unaosababisha vifo vyao. Naye Freda kwa upande mwingine amesawiriwa kama msichana mwadilifu anayejiunga na huduma ya usista pamoja na taaluma ya uuguzi ili

kumhudumia Mwenyezi Mungu na wagonjwa. Katika kuwahakiki wahusika hawa wa mraba mmoja ama miraba minne tunalosema ni kwamba sifa hizi hujitokeza tu tunapomzungumzia mhusika fulani kimaudhui. Kwa mfano tunapomhakiki mhusika mkuu au msaidizi ndipo tunapoweza kumwangazia na kudai kama yeye ni wa miraba minne au mmoja.

## 2.7. Wahusika Jumui

Hawa ni wahusika ambao wamefumbata na kuwakilisha sifa za wahusika wengi, yaani ni wahusika ambao ndani yao wanakuwa na sifa za wengine wengi. Aghalabu wahusika kama hawa watakuwa ndio wahusika wakuu. Katika riwaya ya *Vipanya Vya Maabara*, Bob ametumiwa kama kielelezo cha vijana wengi na matatizo ambayo yanawakumba. Baadhi ya matatizo haya ni kama vile wazazi ambao hawawajibiki, matatizo ya ukosefu wa ajira, uraibu unaohusiana na matumizi ya vitafunaji kama miraa, mambo yanayohusiana na kufanya mapenzi kiholela pamoja na swala la uekezaji miongoni mwa vijana. Uchunguzi wa wahusika wengi katika riwaya hii unaonyesha kwamba wengi wao hawajastawishwa kwa kina ili kutuwezesha kuwachambua kikamilifu ila Bob ambaye ndiye mhusika mkuu anayewakilisha "uso" wa vijana katika jamii ya kisasa pamoja na changamoto ambazo zinawakumba na namna wanavyofaa kukabiliana na changamoto hizo. Yaani kupitia kwake tunafahamishwa ni mkabala upi ambao vijana wanafaa kuchukua ili kuhakikisha kwamba hawaangamizwi na changamoto hizo.

## 2.8. Wahusika wa Kimapinduzi

Kimsingi hawa ni wahusika ambao katika vitendo vyao wanaonyesha mwamko mkubwa juu ya utu na utambuzi wa wito wao na wajibu wao wa kupigania haki za watu wao kwa kuleta mabadiliko chanya katika siasa, uchumi na hata maslahi ya kijamii kwa wote. Hata hivyo maelezo hayo yanaweza kufarisiwa kwa misingi tofauti ambapo katika mapinduzi hayo, mabadiliko katika fikra na mienendo ya watu ndilo jambo muhimu. Katika uhakiki huu wa

uanishaji wa wahusika, tungependa kusema kwamba ujumbe muhimu ambao mwandishi anataka kuzua ni kwamba mapinduzi yanahitajika katika mstakabali wa vijana maishani mwao. Huenda Bob asiwe ni yule mhusika wa kimapinduzi anayejitokeza na kubainika bayana kama mpinzani wa dhuluma fulani katika jamii kama afanyavyo Mwelusi katika *Kifo Kisimani*. Kunayo mapinduzi ya kimawazo ambayo vijana wanafaa kuzingatia. Kwanza Bob hakubagua kazi, alikuwa tayari kukabiliana na yoyote ambayo Mungu alimjalia. Na ndipo Vera alipomwuliza ni kazi gani angependa kufanya, alisema ni yoyote (*Vipanya vya Maabara uk 4*), uwe ni ukarani, polisi au hata uendeshaji gari. Vijana wengine wangekuwa na hali ya kubagua kazi huku wakiziona kazi zingine kama duni.

Hatua nyingine ya kimapinduzi ambayo mhusika Bob alitekeleza ni busara kubwa ambayo alionyesha katika matumizi ya fedha zile alizozawadiwa. Kwa msingi vijana wanapopata pasa kama hizo, huingiwa na kiwewe na kubobea katika maisha ya anasa hivi kwamba wanagutuka baada ya kufuja kiasi kikubwa cha rasilimali yao. Kwa hivyo namna ambavyo Bob aliwekeza kwa busara unafaa kuleta mapinduzi katika fikira ya vijana. Ili wawe waangalifu katika matumizi yao ya kifedha na kuepukana na ufujaji wa mali bali wawekeze kwa manfaa yao ya siku zijazo. Tungependa kusema kwamba si Bob pekee ambaye anawakilisha mapinduzi hayo. Jamila vilevile anachangia kutokana na uamuzi wake kuhusiana na masharti ya wazazi wake kuhusiana na kutotangamana kimapenzi na mtu asiye wa dini yake ya Kiislamu.

### 2.9. Wahusika wa Kisaikolojia

Huu ni uanishaji ambao umependekezwa nao Mlacha na Madumula (1989). Aina hii ya wahusika inaweza kutambulika kutokana na usawiri wake ambao unamwasilisha katika hali ya unyonge na kukata tamaa kwa ajili ya matatizo yanayomkumba katika jamii na kumdhalilisha kiasi cha hata kuhurumiwa na jamii. Hali hii inaweza kutokana na familia yake

kushindwa kumkidhia mahitaji yake na hatimaye kumfanya akumbwe na matatizo mengi sana katika jamii. Yamkini anaitwa wa kisaikolojia kutokana na matatizo yanayomkumba kumfanya ahurumiwe na jamii. Tunaweza kudai kwamba mhusika mkuu wa *Vipanya Vya Maabara* Bob Kerogo anastahili kuingizwa katika kundi hili kwa sababu ya dhiki ambazo zinamkumba katika masomo yake. Baada ya babake kuingilia ulevi, masomo yake yaliathirika. Alikuwa na uwezo wa kufanya vyema zaidi lakini kutokana na matatatizo ya karo yaliyomkumba hakuweza kuhudhuria masomo yake ipasavyo na hivyo kushuka kabisa katika kiwango chake cha masomo. Ilibidi yeye na dadake wategemee wahisani kama vile mjombake Mbaabu pamoja na Padre Giovani. Lakini haimaanishi kwamba mhusika wa kisaikologia hawezi kuwa na sifa za makundi yale mengine mengine. Aghalabu wahusika hawa wa kisaikolojia huwa ni wahusika wakuu na ndipo dhiki zile wanazozipitia zikawa na athari kubwa katika jamii.

### 2.10. Wahusika wa Kiupelelezi

Tunagusia swala la wahusika wa upelezi kwa sababu aina hiyo ya wahusika wamehusika katika *Vipanya Vya Maabara* ambapo katika kuimarisha upelelezi wa kupata kujua mwuaji wa mwanawe, Seneta Humprey King alihusisha majasusi wawili wa F.B.I katika uchunguzi huo. Hata hivyo wahusika wenyewe hawajapewa nafasi pana ya kutuwezesha kuwaelewa vyema. Katika fasihi ya Kiswahili, waandishi wawili ambao wamefaulu kutumia wahusika wa kipelelezi ni Mohamed Said Abdalla ambaye mhusika wake mkuu huwa ni Bwana Msa, mpelelezi mwenye ujuzi mkubwa wa kupeleleza na kuchunguza kesi za jinai zikiwemo mauaji ya kutatanisha kama vile katika *Kisima cha Giningi* (Mohamed 1960). Hata hivyo Bwana Msa amebuniwa kwa kuiga mbinu za upelelezi za Sherlock Holmes ambaye ni mhusika aliyebuniwa na mwandishi wa bunilizi wa Uingereza aitwaye Arthur Conan Doyle. Mbinu anazotumia Sherlock Holmes zinafanana na Bwana Msa katika kuwafikia wahalifu. Mwandishi mwingine ambaye amechangia pakubwa katika matumizi ya mhusika wa

kiupelelezi ni Mtobwa wa Tanzania ambaye amefaulu kumbuni mhusika mpelelezi Joram Kiango. Baadhi ya kazi zake Mtobwa zenye upelelezi huo ni kama vile *Dar-es-salaam Usiku* na *Zawadi ya Ushindi*. Ingawa katika *Vipanya Vya Maabara* majasusi hao hawakupewa nafasi kubwa. Katika kazi zake Mohamed Said Abdalla, Bwana Msa anachukua sehemu kubwa sana kama mmoja wa wahusika wakuu.

### 2.11. Wahusika Duara, Bapa na Shinda

Hizi ni dhana za uanishaji wa wahusika kwa kuzingatia uthabiti wa misimamo yao katika mwingiliano wao na wahusika wengine ambao wana mtagusano nao katika mazingira hayo.

#### 2.11.1 Wahusika Duara

Hawa ndio wahusika ambao sifa zao zinakaribiana zaidi na binadamu wa kawaida yaani wanaonyesha uhalisia zaidi, kwa vile wanaweza kubadilika kimawazo, kitabia au kisaikolojia kutegemea hali ya maisha au mazingira ambamo wanaishi.Wahusika wa aina hii huwa ni wa miraba minne. Uduara wao umo kwenye mabadiliko yanayowajia. Uduara unaweza kuwahusu wahusika wakuu na hata wasaidizi. Kwa mfano Maimuna katika riwaya ya *Utengano* anaonyesha sifa za uduara. Alipoondoka kwao ili kuepukana na hali ya kutawishwa na babake mradi apate uhuru, hatimaye aliishi maisha ya ukahaba. Lakini hali hiyo ya maisha ilipomshinda alisalimu amri na kuanza maisha mapya kwa kuolewa na Kabi mvulana maskini ambaye nyanyake Bi. Farashuu alikuwa ni hasimu wa babake Maksuudi.

Wahusika duara ndio wanaonyesha mienendo ambayo inakaribiana sana na binadamu wengi katika hali yao ya kila siku. Hivi ni kusema kwamba wahusika wa aina hii wana uhalisia zaidi. Katika *Vipanya Vya Maabara* Freda hakuwa na lengo la kuwa mtawa. Aliugeukia uamuzi huo baada ya mpango wake wa awali wa kujifunza uhazili, uwekaji hesabu za fedha na kompyuta kugonga mwamba kutokana na uhaba wa kifedha. Na kwa hakika hivi ndivyo

hali halisi ya maisha ilivyo. Watu hubadili mipango yao ya awali maishani kutokana na misukumo ile inayowakumba na hata pengine kutokana na ushauri au ushawishi wa watu wengine. Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba wahusika duara ndio wenye uhalisia na uyakinifu zaidi katika fasihi.

### 2.11.2 Wahusika Bapa

Hawa ni wahusika ambao huumbwa maksudi na mwandishi au msanii kwa lengo fulani maalum. Yaani mtunzi anaamua kuwasawiri hivyo kwa madhumuni ya kutimiza wazo fulani. Katika uhakiki, wahusika bapa huwa hawabadiliki yaani wakibuniwa kama wazuri basi wanadumisha uzuri wao hadi mwisho na vilevile wakiiumbwa kama wabaya vivyo hivyo wanadumisha ubaya huo hadi mwisho wa kisa. Hii basi ina maana ya kwamba wahusika wa aina hii huwa ni wa mraba mmoja. Katika kundi hili la ubapa, wahusika hao wanaweza kuwa ni *bapa sugu* yaani wale ambao sifa zao tunazipata kutokana na maelezo tunayopewa na msanii kuwahusu au wanaweza kuwa ni *bapa vielelezo* yaani wanaweza kupewa majina ya kimajazi ambayo yanadhihirisha sifa zao.

Wahusika bapa vielelezo kama walivyo wahusika bapa sugu huwa hawabadiliki. Katika kazi zake Mohamed Said Abdalla, Bwana Msa ni mhusika bapa. Vilevile katika *Vipanya Vya Maabara* , Swaleh, Kamash, Muli, na hata Rashid Hamisi ni wahusika bapa kwa sababu katika vitendo vyao hakuna uzuri wowote ambao msanii amenuia kuwapa. Tunachoweza kusema katika uhakiki huu wa wahusika ni kwamba, wahusika bapa ni wa kinadharia tu kwa sababu katika maisha ya kila siku, si kawaida kwa mtu kuwa na sifa hiyo moja ya ubaya pekee au uzuri pekee. Watu kwa kawaida huwa na tabia changamano huku kila tabia ikijitokeza kutegemea hali iliyopo.

### 2.11.3. Wahusika Shinda

Wahusika shinda wanaweza kuzungumziwa tu pale ambapo kuna wahusika bapa na wahusika duara yaani wapo baina ya wahusika bapa na wahusika duara. Hii ina maana kwamba kuwepo kwao hutegemea makundi hayo mawili, yaani wanapelekwa mbele kutokana na mawazo pamoja na tabia za wahusika hao wengine. Hii ina maana kwamba iwapo mtagusano wake unaegemea upande wa wale bapa basi ataonyesha sifa zile na iwapo anasukumwa zaidi na wale duara basi vivyo hivyo, ataegemea upande wa uduara. Tungependa kudai kwamba mhusika kama Muli alikuwa ni wa aina hii kwa sababu wakati alipokuwa na vijana wenzake waadilifu kama vile Bob na Okach, tabia zake zilikuwa adilifu lakini akiwa mbali nao alikuwa ni mtumiaji sugu wa madawa hayo ya kulevya. Tunachotaka kusema vilevile ni kwamba wahusika shinda wapo katika jamii huku wakikosa msimamo na kufuata tu upepo kutegemea kule waliko.

## 2.12. Wahusika Vijana

Tatizo la utafiti wetu ni kuhakiki hali ya vijana katika *Vipanya Vya Maabara* na kwa sababu hiyo, uanishaji wa wahusika hautakuwa kamili bila kuliangazia kundi hili muhimu. Waandishi wengi siku hizi wanatambua umuhimu wa vijana na ndipo maandishi yao yakawa yanawamulika sana vijana. Tulieleza katika utangulizi kwamba kiwango cha ujana kinatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine lakini kulingana na sera ya kitaifa, kijana ni mtu yeyote ambaye umri wake ni baina ya miaka kumi na mitatu na ishirini na minne. Sehemu kubwa ya wahusika wa *Vipanya Vya Maabara* ni vijana wakiwemo Bob ambaye ni mhusika mkuu, Okach, Jamila, Freda, Swaleh, Wairi, Muli, Kajuju, Achieng, Gaceri. Uhusika wa vijana katika riwaya hii ni muhimu kwa sababu mwandishi anatathmini shida ambazo zinawakumba. Tungependa kusema kwamba vijana wametumiwa kama wahusika wa kiuamilifu yaani kama vyombo vya kutimiza dhamira yake mwandishi.

Katika *Vipanya Vya Maabara,* changamoto zinazowakumba vijana ndilo lengo kubwa ambalo mwandishi alikuwa nalo na alitaka kulitimiza kupitia kwa vijana wenyewe. Tukiwaangalia vijana hawa kiutendaji katika nafasi wanazozichukua basi ndipo tunapobaini uamilifu wao. Changamoto wanazozipitia ni nyingi mno. Lakini bado kuna uwezekano wa vijana kukabiliana nazo na kufaulu maishani. Amewatumia vijana vilevile kama chombo cha matumaini ya kuondoa ukabila nchini kwa vile tunawashuhudia wakitangamana bila kujali makabila yao. Tunakamilisha uhusika wa vijana kwa kusema kwamba Bob ndiye anayeibuka kama mhusika shujaa. Anawapa matumaini vijana wenzake na kuwafanya wasife moyo kwa sababu mabadiliko yanaweza kuwajia maishani mwao.

### 2.13. Wahusika Viongozi

Hawa ni wahusika ambao wanashikilia nyadhifu za uongozi serikalini au hata katika jamii. Wao ni muhimu kwa sababu sera zinazowaathiri vijana zinabuniwa nao.Vilevile wanatarajiwa kuwa kielezo kizuri sana kwa serikali hiyo wanayoihudumia. Lakini hivi sivyo ilivyo. Badala yake wanafanya vitendo ambavyo ni kinyume kabisa na matarajio ya jamii. Waziri Rashid Hamisi anawakilisha viongozi hao. Kwa kweli vitendo vyake ni vya kuiaibisha na vinatoa sura mbaya sana kwa serikali hiyo anayoihudumia kwa kujihusisha na vitendo vibaya sana vya uzinzi, ulanguzi wa madawa ya kulevya na hata mauaji.

### 2.14. Wahusika Wazazi

Familia ni asasi muhimu sana katika jamii na inatarajiwa kubuni mazingira bora ya kuwezesha malezi bora ya watoto.Katika asasi hii, wazazi ndio msingi wake; wanapokosa kutekeleza wajibu wao ipasavyo basi vijana ambao wanahitaji sana uelekezi wao wanajikuta taabani bila mwongozo bora maishani. Katika *Vipanya vya Maabara*, wazazi wameshindwa kutimiza wajibu wao wa kutoa malezi bora na ndipo wanao wanakumbwa na matatizo mengi. Inspekta Fadhili na mkewe hawana nafasi ya kumshauri mwanao Swaleh na ndipo anaishia

kuwa jambazi. Sajini Njoroge na mkewe wanakosa nafasi ya kumwelekeza mwanao Wairi na kumwachia uhuru mwingi sana. Matokeo ni kwamba hatima yake ni ukahaba.

### 2.15. Wahusika Vinyago au Kerekecha

Wahusika kerekecha huumbwa kwa namna ya kimzaha ya kuwafanya wale wanaoisoma kazi hiyo wacheke. Lakini lengo la msanii la kumsawiri mhusika hivyo katika hali ya kudhihaki na kukejeli huwa si kuchekesha tu bali huwa ni kutuchochea ili tubaini udhaifu uliomo katika uhusika wa mhusika huyo ili tupate funzo fulani baada ya kutafakari kuhusu hali ya mhusika mwenyewe. Katika *Vipanya vya Maabara* kunao wahusika ambao ni wa aina hii. Kwa mfano Rashid Hamisi ameumbwa kama mhusika kerekecha. Anaiaibisha wizara ile ambayo anasimamia kama waziri kwa kutenda mambo ambayo hayafai kutendwa na mtu wa cheo chake. Badala ya kuwa kielelezo bora cha uwaziri anakuwa ni kichekeleo kwa kujihusisha kimapenzi na makahaba kama Wairi, anayalangua madawa ya kulevya kwa kuwashirikisha vijana kama Swaleh katika biashara hiyo haramu. Isitoshe anamwua Rita King baada ya kumbaka. Sisi kama wasomaji tunapomwona mhusika kama Rashid, Waziri wa Wizara yenye ushawishi mkubwa kama hiyo akijihusisha katika matendo ya aina hiyo tunabaki tukijiuliza ni kwa nini viongozi wasiwe ni vielelezo vya kuigwa. Konstebo Kerogo naye anakuwa ni mhusika kerekecha au kinyago kwa ajili ya kuiaibisha taasisi ya ndoa na familia.

### 2.16. Mhusika wa Kihalisi

Wamitila (2008;387) anawaeleza wahusika kihalisi kama wale ambao sifa zao zinashabihiana sana na binadamu katika hali yake ya kawaida. Yaani ni wahusika ambao vitendo vyao vinafanana sana na vya binadamu wa kawaida. Hii ina maana kwamba iwapo ni mhusika kijana vitendo vyake vifanane na vya kijana na vikubalike. Kwa mfano vitendo vyake kijana Bob Kerogo vya kufanya ngono ovyo ovyo na kutafuna miraa kila jioni katika eneo la Tea Room jijini Nairobi vina uhalisia kwani vijana wengi hufanya hivyo.

### 2.17. Hitimisho

Wahusika huwa wanasawiriwa na mwandishi kwa njia mbambali kutegemea lengo lile ambalo mwandishi huyo anataka kutimiza. Usawiri wa wahusika hao ni swala changamano ambapo huweza kuwa na mwingiliano mkubwa kati ya mhusika mmoja na mwingine. Kwa sababu hii, uainishaji si jambo rahisi. Ugumu huu hutokana na mwingiliano huu wa sifa. Kwa mfano, tunapomtambua mhusika fulani kama mhusika mkuu, huenda vilevile akawa ni bapa kielelezo, duara, wa kimapinduzi na kadhalika. Lakini huu ndio uhalisi wa mambo kwa sababu hakuna mhusika ambaye anaweza kuwa na sifa moja tu. Kwa sababu akiwa hivyo basi atakosa uhalisia. Jambo lingine muhimu kutaja hapa ni kwamba hakuna njia moja maalum ya kuainisha au makundi maalum ya uanishaji ambayo hayabadiliki.Uanishaji unategemea mkabala wa mhakiki huyo pamoja na aina ya kazi ambayo anayoihakiki pamoja na wahusika waliyomo. Tunaamini kwamba uainishaji ambao tumefanya katika sura hii utatusaidia sana katika kuwahakiki wahusika wenyewe katika sura zijazo pamoja na matatizo mbalimbali yanayowakabili.

# SURA YA TATU

# UHAKIKI WA WAHUSIKA

## 3.0. Utangulizi

Katika sura hii, tuliwahakiki wahusika, hususan vijana kwa kuwahusisha na makundi ya uhusika tulivyoyajadili katika sura ya pili, uhakiki wenyewe ulijikita katika nadharia ya uhalisia. Wamitila (2003) anamweleza mhusika kama kiumbe anayepatikana katika kazi ya fasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Anaendelea kudai kwamba wasifu wa mhusika unategemea mkabala uliopo; ambapo kazi ambazo zinaegemea mitazamo ya uhalisia zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida.

Tunakubaliana naye Wamitila kwamba wasifu wa mhusika utategemea mkabala wa msanii anayemuumba na kumsawiri. Kwa mfano mhusika ambaye anasawiriwa kwa misingi ya uhalisia ajabu kama vile Bina Adamu msafiri katika riwaya ya *Bina Adamu* ya (Wamitila 2009) hana uhalisia wa kawaida kamwe. Mhusika kama huyu anasawiriwa katika hali ya uajabu fulani na uwezo wa kutenda matendo fulani ambayo si ya kawaida. Kwa mfano katika *Bina-Adamu,* *y*ule *Bina-Adamu* msafiri katika safari yake yakuwatafuta wale mahuntha watatu alipitia mazingira yasiyokuwa na uhalisia, lakini wahusika waliobuniwa katika misingi ya nadharia ya uhalisia wanatakiwa kuwa na ushabihi ukweli. Yaani ni lazima matendo yao au sifa zao kwa jumla zifanane na zile za binadamu wa kawaida. Hii ina maana kwamba akiwa ni kijana, mzee, mama au mtoto ni lazima mienendo yake ifanane na ujana, uzee au utoto.

Mazingira yanayotumiwa ni lazima yaafikiane na matendo ya wahusika hao. Kwa mfano iwapo mhusika anayesawiriwa ni mhadhiri wa chuo kikuu ni lazima mazungumzo yake yaonyeshe uhalisia ambao unalingana na usomi wake na kumtofautisha na mwenzake

anayeishi mashambani na ambaye kisomo chake ni cha hali ya chini. Usawiri mwafaka wa mhusika kwa hivyo,ni muhimu sana kwa sababu unachangia pakubwa ufanisi wake msanii au mwandishi katika kuyatimiza maudhui yake. Riwaya ya *Vipanya vya Maabara* kwa yakini imehusisha kwa kiasi kikubwa sana wahusika vijana ambapo maudhui mengi yanawahusu. Katika tasnifu hii tumeangazia sifa za vijana wote waliohusishwa katika riwaya hiyo pamoja na umuhimu wao pamoja na matatizo yanayowakumba.Mbali na vijana tumewashughulikia vilevile wahusika wengine wasio vijana na wanaochangia katika kuwajenga vijana hao na hasa baadhi ya matatizo yanayowakumba.

### 3.1. Bob Kerogo

Yeye ni mvulana wa umri wa miaka ishirini na mmoja ambaye alifikia upeo wa elimu ya kidato cha nne. Ni mwanawe Konstebo Kerogo afisa wa polisi katika kituo cha polisi cha Bondeni, mamake ni Maria, dadake ni Freda. Kimo chake ni kirefu na na ana umbo la kuvutia. Umuhimu wake Bob ni kwamba ametumiwa kama kielelezo cha kuonyesha masaibu yanayowakumba vijana ambao wamepitia mfumo wa elimu wa nane nne nne na hasa changamoto zinazowakabili, si katika mambo ya ajira tu bali pia mashinikizo mengine ya kijamii pamoja na ufaafu wa mfumo wa elimu ya 8 - 4 - 4.

Bob ndiye mhusika mkuu katika riwaya hii kwa sababu mbali na ukweli kwamba hadithi inamhusu yeye, ndiye tena msimulizi wa hadithi yenyewe. Bila shaka tukimwondoa Bob katika hatua yoyote ya hadithi hii basi itakwama na haitaendelea tena. Kwa upande wa uhusika wake, mbali na kuwa mhusika mkuu.Yeye ni jira ya kazi hii; (Wamitila: 2008) kama asemavyo Wamitila (2008). Vile vile ana sifa ya uduara yaani anabadilikabadilika kulingana na hali ambayo inamzingira kwa wakati Fulani. Hii ni sifa muhimu sana katika mhusika mwenye uhalisia. Yaani katika hali ya uhalisia mtu hubadilika kulingana na hali ambayo inamkabili. Vilevile tunaweza kumweleza kama mhusika msimulizi kwa sababu ni yeye

mwenyewe anayekisimulia kisa chake katika nafsi ya kwanza...........*Tukio la kukutana kwangu na Vera lilipeperushwa na upepo wa bahati hadi mkononi mwangu* ......(uk 1). Kwa jumla, Bob akiwa mhusika duara kama tulivyodai hapo awali ana sifa chanya na vilevile hasi kwa sababu hiyo ndiyo hali halisi ya binadamu wa kawaida ambaye ni muhali kuwa mkamilifu kamili.

Sifa ya kwanza ambayo Bob alionyesha ni kuthamini na kufurahia kazi yoyote aliyojaliwa. Kwanza kabisa kazi aliyokuwa akifanya baada ya kuhitimu kidato cha nne ni kuosha magari. Alifanya kazi hiyo kwa uangalifu mkubwa. Vera alimpomletea gari lake amwoshee, alifanya kazi hiyo kwa makini sana hadi Vera mwenyewe akafurahia kazi aliyoifanya. Vera alipompa kazi ya kuendesha gari lake, alifurahia sana. Alihakikisha kwamba alidumisha hali ya nidhamu na kuliendesha gari polepole. Hata hakuthubutu kuongea naye mwajiri wake hadi alipofika kizingo cha uwanja wa Nyayo ambapo hakukuwa na msongamano wa magari ndipo alipotulia. Hata wakati Vera alipomwuuliza ni kazi gani ambayo angependa kufanya, alisema kwamba angeifanya kazi yoyote iwe ni ukarani, polisi au udereva (uk 4). Isitoshe wakati mjombake alipomtafutia kibarua kwa rafiki yake mhindi Devji alifanya kwa moyo wake wote. Ingawa ilikuwa nzito aliifanya bila kulalamika.

Sifa nyingine chanya ambayo Bob alikuwa nayo ni ilhamu ya kusoma. Tangu umri wa miaka 14 Bob alisoma kwa undani na kwa upana akawa na uelewa mpana sana kuhusu matukio ya kimataifa. Aliyasoma magazeti na hata akalipia uanachama wa maktaba kwa mwaka mzima ili apate kusoma kwa mapana ili aelewe matukio ya kimataifa kwani huu ni msingi muhimu kwa vijana kuelewa namna misikumo ya mataifa haya yenye ushawishi mkubwa duniani inavyoathiri mataifa maskini. Hii ni sifa ambayo vijana wanastahili kuiga. Bob ni mwaminifu. Aliwahi kukopa pesa kutoka kwake Wairi, lakini siku alipomfanyia Vera kazi ya kumwooshea gari na kulipwa shilingi mia mbili alikumbuka kumlipa Wairi deni lake.

Uaminifu huu vile vile ulibainika wakati alimrudisha Vera hadi Karen ambapo Vera alipomwuuliza ni kiasi gani cha fedha alitaka alipwe alisema mia mbili; vijana wengine wangedai kiasi kikubwa zaidi eti kwa sababu alikuwa mzungu. Vilevile siku ile alimpeleka Vera na mpenzi wake Larry Johnson kuzuru Ziwa Nakuru, ikiwa ndiyo siku ambayo waziri Rashid alimwua Rita King, Bob aliokota pochi yake marehemu Rita King iliyokuwa na dola za marekani lakini hakuchukua chochote mle ndani.

Bob anajiamini na ni jasiri. Kwa mfano alipokutana naye Vera mara ya kwanza hapo Safari Hotel, aliongea na huyo mwanamke mzungu kwa njia huru kabisa bila uoga. Vijana wengine wenye umri mdogo kama huo wa miaka 21 wangeonyesha uoga hasa wakikutana na wazungu. Bob ni mkarimu. Jambo hili linabainika siku ile ambapo walizuru Kitengela na Wairi, Swaleh na Waziri Rashid. Kati ya shilingi mia tano ambazo Rashidi alimpa Bob ili "amruhusu" kubaki na Wairi, Bob alimpa Swale shilingi mia mbili.

Ni kijana aliyewajibika. Muda ule ambao alipata kibarua katika duka la Devji aliweza kuwajibika kwa kugharamia mahitaji ya nyumbani kwao. Sifa moja chanya ya kujivunia zaidi kumhusu Bob ni namna alivyowekeza kitita cha shilingi milioni sabini alizotunukiwa baada ya kumtambua mwuaji wa Rita King bintiye Seneta King wa Marekani. Alinunua nyumba ya kifahari huko mtaa wa Mlimakuu. Vilevile alinunua Safari Hotel kiushirika na mjombake Mbaabu, na akajenga nyumba za kifahari za kukodesha huko Kileleshwa. Alimuajiri wakili mwenye sifa yaani Okach ili kusimamia biashara zake kisheria. Kwa jumla nidhamu aliyokuwa nayo Bob kuhusu fedha tangu ujana wake ni ya kuigwa na vijana. Uwekezaji aliofanya na pesa hizo ulikuwa ni wa busara na wa kumhakikishia pato zuri daima. Vijana wengine wa umri huo wangetumia pesa hizo kwa ubadhirifu kwa njia ya anasa.

Bob akikuwa na mlahaka mzuri sana na vijana wenzake. Alishirikiana kwa karibu sana na mahirimu wenzake kama Jamila, Swaleh, Okach, Wairi, Muli na wengineo. Hatimaye alimwoa mpenzi wake wa utotoni Jamila na katika kufanya hivyo akavunja mipaka ya kidini iliyokuwa imewekwa na wazazi wake Jamila waliokuwa waislamu wa itikadi kali. Licha ya sifa hizi chanya ambazo tumemtunukia, Bob alikosa nidhamu upande wa mapenzi. Alifanya mapenzi kiholela huku akihusiana naye Jamila, Gaceri na hata Vera. Hii ilikuwa tabia hatari ya kuweza kumletea maradhi kama ukimwi. Hata baada ya kuoa aliendelea kufanya mapenzi kisiri na Vera.

Tabia nyingine hasi ambayo Bob alionyesha ni uraibu wake wa miraa. Kile jioni baada ya shughuli zake, hakuna siku aliyokosa kupitia Rivarodi au eneo la Latema Road kununua Miraa. Labda tabia nyingine hasi ni ile ya kuiga tabia za kimagharibi. Shuleni mwake yeye ndiye alikuwa na ustadi wa mchezo wa mpira wa vikapu na hivyo basi akawa ananyoa nywele zake mtindo wa Michael Jordan. Isitoshe, Bob yu tayari kunufaika kutokana na mali ya wizi au haramu. Kwa mfano yeye alijua wazi kwamba Swaleh alikuwa ni mwizi wakimabavu. Lakini licha ya hayo alikuwa tayari kununuliwa pombe kutokana na mali ya wizi. Na ndipo anamweleza Swaleh (uk 13)..................... "Kwa hivyo leo utakuwa na mfuko mzito. Tutakutania wapi unirushie kanywaji kamoja."

### 3.2. Vera

Huyu ni mwanamke mzungu. Alikuwa ni mjane wa mwanamume mzungu marehemu J.C. White ambaye aliuawa na majambazi na kumwachia mkewe utajiri mwingi. Hawakuwa na watoto na waliishi katika mtaa wa kifahari wa Karen jijini Nairobi. Vera ni mojawapo wa wahusika wakuu katika riwaya hii kwa sababu uhusiano wake na Bob unaanza tangu ukurasa wa kwanza hadi mwisho wa kisa. Uhusika wake umezagaa katika kisa kizima. Ufanisi wake Bob hatimaye maishani mwake ulitokana na uhusiano wake na Vera. Katika mienendo yake,

Vera anadhihirika kama mhusika bapa sugu. Kamwe habadiliki katika uhusiano wake na Bob. Tangu wakutane huko Safari hotel, Vera hakubadilisha hali yake ya kuhusiano naye Bob. Akiwa na mpenzi wake Larry Johnson, Bob alikuwa ni dereva tu lakini wakiwa pekee yao Bob alikuwa ni mpenzi. Isitoshe hakuna wakati ambapo Vera alithubutu kumudhibiti Bob na kummiliki maishani mwake. Alikuwa akimtumia tu alipomhitaji kwa shughuli maalum. Hata baada ya Bob kumwoa Jamila, waliendelea kuhusiana kimapenzi kisirisiri.

Umuhimu wake katika riwaya hii ni kwamba uhusiano wake na Bob Kerogo ndio uliyobadilisha maisha ya Bob. Hii ni kwa sababu mbali na kumlipa vizuri kila alipomwooshea gari lake, Vera alimpa kibarua cha kumwendesha katika gari lake mara kwa mara. Na ni kutokana na mojawapo ya ziara hizo katika mbuga ya kihifadhi wanyama huko ziwa Nakuru ambapo kwa sadfa, Bob alishuhudia tukio ambalo liligeuza maisha yake daima katika siku za usoni. Aliweza kumfumania waziri Rashid akiuburuta mwili wa mwanamke mzungu na kumweka ndani ya sehemu ya nyuma ya gari lake na kwa silka na tuhuma akapiga picha mbili nzuri za tendo hilo. Ilisadifu kwamba mwanamke huyo alikuwa ni Rita King bintiye Seneta Larry King wa Marekani. Kifo hicho kilizua upelelezi mkali, huku serikali ikijitahidi kufichua ukweli.

Hatimaye Seneta King alitangaza zawadi ya dola milioni moja, sawa na shilingi milioni sabini za Kenya. Bob ndiye aliyenyakua pesa hizo kwani alikuwa na ushahidi thabiti kuhusiana na tukio hilo kwa sababu alikuwa na picha safi alizozipiga zikionyensha waziri aking'ang'ana na mwili wa mwanamke huyo.

Kuna wale ambao wanaweza kumchukulia Vera katika hali hasi. Wanaweza kudai kwamba umuhimu wake ni kuwa yeye ni kielelezo cha wanawake wajane matajiri. Wanawake kama hawa hutumia mali yao ili kuwanasa vijana wakembe chipukizi ili wafanye mapenzi nao. Mfano mzuri ni ule wa Vera. Alitumia nafasi aliyoipata alipozuru hifadhi ya wanyama ya

Ziwa Manyara nchini Tanzania kumshawishi Bob kufanya mapenzi naye. Kwa upande wa sifa, Vera ana sifa kadhaa. Kwanza anajitokeza kama mwanamke mkarimu sana. Bob alipomwoshea gari lake mara ya kwanza, alimlipa shilingi mia mbili, tofauti na shilingi ishirini ambazo ndizo alidai kwa kuosha kila gari. Isitoshe baada ya kumwoshea gari, Bob alikaribishwa na mama huyo ndani ya hoteli na hata akamnunulia pombe. Ni mwanamke mzungu ambaye hakuwa na ubaguzi. Kwa mfano wazungu wengi aghalabu hujithamini na kujiona bora kuliko wafrika na kwa hivyo huwa hata hawapendi kutangamana nao hadharani.

Vera alikuwa ni tofauti sana licha ya kwamba Bob alikuwa ni dereva wake tu, Vera alihusiana naye kana kwamba walikuwa ni sawa katika hadhi. Katika mahali pa starehe kama Safari Hotel, Vera alitangamana naye Bob hata wakakaa meza moja akimnunulia pombe. Wakati Bob alipomwendesha kwa gari lake hadi Karen, alimkaribisha kwa ukarimu mkubwa na hata chakula alichoandaa cha maini walikila katika sahani moja wakitumia uma mmoja. Wengine wenye hadhi kama ya Vera wangemtenga kando ili ahudumiwe peke yake.

Vera ni mwanamke mwenye hekima na msiri sana. Tangu akutane naye Bob mara ya kwanza huko Safari hotel, alimpenda lakini hakulifanyia pupa jambo hilo. Alilipeleka hatua kwa hatua hadi wakati ambapo alipanga safari ya kwenda naye ziara ya nchini Tanzania ndipo alimfichulia hisia zake katika hoteli ile walimokuwa. Na hata baada ya hapo, Vera hakuonyesha wazi kiwewe cha mapenzi kwake Bob. Hata wakati walipozuru ziwa Nakuru wakiwa na Harry Johnson mpenzi wake Vera, hakukuwa na dalili yoyote kwamba kulikuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi baina ya Vera na Bob. Vera alikaa na mpenzi wake nyuma ya gari wakifanya yao huku Bob akishugulika na usukani. Naye vilevile alionyesha ukomavu wa kutobainisha wivu wa kihisia.

Hakuna binadamu aliye mkamilifu. Licha ya sifa hizi chanya ambazo tumemlimbikizia mama huyu mzungu, bila shaka ana chache ambazo ni hasi. Kwanza kabisa, anaonyesha tabia za ukware, ingawa ana mpenzi wake Larry Johnson vilevile anasalitika kimapenzi na Bob. Kitendo kile alichokitenda katika ukingo wa Ziwa Manyara nchini Tanzania vilevile kilionyesha utovu wa maadili. Alizivua nguo zote na kubaki na chupi ili Bob apate kumpiga picha. Kitendo hicho kwa hakika ndicho kilichompa Bob hamu ya kutaka kufanya mapenzi na mama huyo.

Anaonyesha tabia za kutojiheshimu. Ni utovu wa heshima kwa mama wa hadhi kama yake kuwanyemelea vijana kama Bob na kufanya mapenzi nao. Ni akina mama kama hao ambao huwavuruga vijana kiakili na kuwafanya wapoteze mwelekeo maishani. Tabia kama hizo zimekithiri sana katika maeneo ya kitalii huko sehemu ya ufuo wa bahari katika mji wa Mombasa ambapo wanawake wazee huwanasa vijana chipukizi na kuwaweka kama waume zao. Basi si ajabu kwa sababu hata Vera alilelewa na kukulia sehemu hizo za Mombasa. Hii ina maana kwamba husika wake Vera una uhalisia mkubwa. Katika jamii yetu kunao akina "mama sukari" ambao hujiingiza katika mapenzi na vijana chipukizi. Kwa mfano mnamo mwaka wa 2003, mjane Wambui Otieno akiwa na umri wa miaka 67 aliolewa na kijana Mbugua mwenye umri wa miaka 27 tu.

### 3.3 Wairi

Anaweza kuainishwa kama mhusika wa mraba mmoja kutokana na sifa kuu ya uzinzi inayobainika kwake. Hii ni kwa sababu akiwa katika kidato cha pili tayari alikuwa mjamzito na kisha hatimaye akawa ni kahaba wa kulipwa Jina lake kamili ni Wairimu, msichana chipukizi bintiye afisa wa polisi Sajini Njoroge wa kituo cha polisi cha Bondeni. Alianza kujihusisha na mapenzi akiwa bado katika shule ya msingi ya Uhuru ambapo tayari aliandamwa na wavulana wengi. Umuhimu wake Wairi ni kwamba yeye ametumiwa kama

kielelezo cha wahasiriwa wa malezi mabaya. Babake Sajini Njoroge na mamake hawakupata nafasi ya kumshughulikia binti yao. Matokeo yake yakawa kwamba Wairi alikuwa na uhuru mwingi sana wa kufanya apendavyo bila ya kuwa na wa kumwelekeza kwa sababu wazazi wake mara nyingi hawakuwepo nyumbani. Wote walijishughulisha na kutafuta fedha zaidi jijini ili kuyakidhi mahitaji yao. Mbali na hali hii ya ulezi Wairi vilevile ametumiwa kama mfano wa vijana chipukizi ambao wanaangamia mapema maishani kwa sababu ya shinikizo zinazowakumba na vilevile kwa sababu ya kukosa mwelekeo bora maishani.

Kwa jumla Wairi anadhihirisha ukosefu wa maadili. Hii inathibitika kutokana na mienendo yake ya kimapenzi. Kwa mfano akiwa katika shule ya upili alikuwa tayari na mlolongo wa wavulana wakimwandama akiwemo Muli ambaye hatimaye alikata tamaa kutokana na ushindani mwingi wa wavulana wengine. Utovu huu wa maadili vilevile ulidhihirika alipotiwa mimba na Bwana Nyamboki, mwalimu mkuu wa shule ya upili ya wasichana ya Moi akiwa katika kidato cha pili na hivyo kukatizwa masomo yake. Hata baada ya kujifungua na kumlea mtoto huyo wa kiume na kisha kumwachia mamake, maisha aliyoyachagua yalikuwa ni yaleyale. Alihamia sehemu za mjini na kuingilia ukahaba kama taaluma yake ya kujiendeshea maisha. Bila shaka kulikuwa na uwezekano wa kujaribu njia bora kuliko kuingilia ukahaba moja kwa moja.

Licha ya hayo, alikuwa ni mtiifu. Kwa mfano wakati alipopata mimba hiyo akiwa kidato cha pili, wazazi wake walipomshurutisha kusema ukweli, alifanya hivyo na hata akatoboa yote kuhusu uhusiano wake na Bwana Nyamboki na hata akafichua barua zote ambazo mwalimu huyo alikuwa akimwandikia.

Wairi alikuwa na mlahaka mzuri sana na vijana wenzake. Haya yalidhihirika wakati alipoandaa dhifa ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa, vijana wote wa Nyayo walihudhuria

yaani Bob, Okach, Muli, Swaleh, Jamila na hata Frida. Jambo hili tena lilidhirihika wakati wa kifo chake, msimulizi anasema kwamba… "hakuna mtu mwingine ambaye mazishi yake yalihudhuriwa na watu wengi kama Wairi..." (uk. 212) Hakuwa na ukabila. Alikuwa ni wa kusema ukweli kwa njia wazi. Kwa mfano, siku Bob alikutana naye. Vera kwa mara ya kwanza alipitia katika danguro alimoendeshea shughuli zake Wairi na wakaweza kuzungumza kwa uwazi sana kuhusu kazi hiyo ya ukahaba pamoja na matumizi ya kondomu na masharti ya malipo. Isitoshe wakati ambapo Wairi alihisi kwamba aliambukizwa ugonjwa huo alimtobolea Bob siri hiyo. Yamkini Bob alikuwa ni kama msiri wake, na ndipo akamwambia Bob, " Nahofia kwamba nimeambukizwa gonjwa hili," (uk 189)

Sifa nyingine aliyokuwa nayo Wairi ilikuwa ni ukarimu. Kwanza kila Bob alipomtembelea, alidhiirisha kuwa mkarimu na kumpa hata whisky. Hata aliwahi kumkopesha Bob pesa. Ukarimu huu pia ulionekana wakati fulani alipompa Freda shilingi moja ili acheze mchezo wa bahati na nasibu wa K.C.S.E. Frida aliposhinda hakumuonea wivu bali walisherehekea pamoja. Katika misingi ya nadharia ya Uhalisia, jambo la wasichana chipukizi kuingilia ukahaba si geni jijini Nairobi. Ni la kawaida kwani katika barabara ya Koinage kuna wasichana chipukizi wanaofika eneo hilo kila usiku kutafuta pesa kwa kushiriki umalaya.Inadaiwa kwamba hata wanafunzi wa Vyuo Vikuu hushiriki. Juzi katika gazeti moja la humu nchini iliripotiwa kwamba wasichana sasa wameanza kutumia mitandao kujibazazi kama makahaba.

**3.4. Jamila**

Huyu anaweza kuelezwa kama mhusika bapa. Wamitila (2003:21) akimnukuu Foster, anamweleza mhusika bapa kama yule ambaye habadiliki tangu mwanzo hadi mwisho wa kisa. Akiwa mbaya atabaki hivyo na akiwa mzuri ni vivyo hivyo. Sababu yetu ya kudai kwamba ni bapa ni kwa sababu alishikilia msimamo wa kukaidi amri ya wazazi wake ya

kutoshirikiana na wasio waislamu. Lakini alipuuza yote hayo kwa kufanya mapenzi na kijana Bob ambaye hakuwa Mwislamu na hata akaolewa naye ingawa wazazi wake walipinga vikali jambo hilo. Hatimaye ilibidi waikubali ndoa yenyewe walipogundua kwamba Jamila hangebadilisha msimamo wake  Alikuwa ni binti na mwana wa pekee wa mwalimu Ramadhan, ambaye alikuwa ni mwalimu mkuu wa shule ya msingi ya Uhuru. Mamake vilevile alikuwa ni mwalimu wa hisabati katika shule iyo hiyo. Alilelewa kwa uangalifu mkubwa sana huku akihimizwa kushikilia dini ya kiislamu na kuonywa kutotangamana na wasio waislamu.

Umuhimu wake ni kwamba yeye ametumiwa kama mfano wa watoto wa kike ambao hudhibitiwa na kutawishwa na wazazi kwa dhana kwamba hayo ndiyo malezi mwafaka lakini badala yake, huwajaza na hamasa ya kujua zaidi, kinyume na matarajio ya wazazi hao. Jamila ametumiwa kama kielezo cha kijana ambaye hataki kufungwa na desturi za kidini au kitamaduni ambazo zinalenga kuwatenga vijana kwa kuwapa masharti fulani ya kufuata katika utangamano wao. Kuhusu sifa zake, Jamila alielezwa kama msichana mrembo sana. Kwa vile alikuwa ni Suriama, huku baba akiwa mwarabu mwenye asili ya Yemen naye mama akiwa Mdigo, Jamila alikuwa ni mrembo na mweupe ajabu.

Alikuwa ni msichana mwenye akili kimasomo kwani baada ya masomo ya kimsingi katika shule ya Uhuru, alifuzu na kujiunga na shule ya upili ya wasichana ya Moi ambapo pia alifuzu katika mtihani wake na kujiunga na chuo kikuu cha Egerton ili kufanya shahada ya B.Sc. ingawa mwenyewe alitaka kufanya uhandisi katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Hii ina maana kwamba mbali na matatizo ya ulezi, Jamila vile vile ni mhasiriwa wa mfumo wa elimu ya nane nne nne ambapo wasomi huteuliwa na Halmashauri ya" JAB" kujiunga na kozi ambazo hawakuzichagua wala kuzipenda. Jamila alijiunga na chuo kikuu cha Egerton shingo upande(uk 115). Si ajabu kwamba baadaye alisomea kozi ya usimamizi wa hoteli ili

kusimamia Safari Hotel ambayo mumewe alinunua pamoja na mjomba wake Mbaabu. Ni msichana mwenye msimamo thabiti. Alikuwa na mapenzi ya dhati kwake Bob ambayo yalidumu tangu siku zao katika shule ya msingi. Hii inathibitishwa na ukweli kwamba, hata wakati Bob alikuwa ni mwosha magari tu na dereva wa muda wa mwanamke mzungu Vera, Jamila hakumdharau ama kwa hali duni ya elimu yake au kazi yake ya kuosha magari. Wasichana wengi baada ya kujiunga na chuo kikuu wangewapuzilia mbali wapenzi wao wa zamani wenye elimu duni na uhaba wa fedha lakini Jamila hakufanya hivyo.

Hata hivyo kuna yale ambayo Jamila alifanya na ambayo yanaweza kuchukuliwa kuwa sifa hasi au mbaya. Kwa kukataa kufuata ushauri wa wazazi wake kuhusu kutofanya usuhuba na wale wasio waislamu, Jamila anaweza kuchukuliwa kama mkaidi. Jambo lingine hasi ambalo alifanya ni namna alivyoupoteza ubikira wake nyumbani mwao katika chumba chake alichopewa na wazazi wake. Ulikuwa ni utovu wa nidhamu wa hali ya juu kumleta mvulana nyumbani mwao ili ambikiri kutoka humo. Isitoshe kupoteza ubikira nje ya ndoa ulienda kinyume na maadili ya mafunzo ya kiislamu. Hata hivyo uaminifu wake kwa Bob ulizawadiwa kutokana na utajiri wa ghafla ambao Bob aliangukia na wakapata kuishi maisha ya starehe ambayo hawakutarajia.Kuna uhalisia mkubwa katika uhusika wake Jamila si katika mambo ya mapenzi tu ambapo vijana wengi hukiuka amri za wazazi na kuolewa na watu waliowachagua wao wenyewe, bali pia hukumbwa na masaibu wakati wa kuchagua kozi katika Vyuo Vikuu.

### 3.5. Freda

Huyu vile vile ni mhusika bapa kwa sababu ya uthabiti wa uadilifu wake kitabia. Hatumshuhudii akishiriki katika uzinzi kama wafanyavyo mahirimu wake kama vile Jamila na Wairi. Licha ya kuwa nao karibu, hafanyi namna wafanyavyo wenzake kwa kushiriki

mapenzi. Ingawa nduguye anamshuku kuwa na uhusiano na Okach, hakuna ushahidi wowote kuhusiana na jambo hili.

Huyu ni dadake mkubwa Bob. Alisomea katika shule ya upili ya Moi huko Limuru. Alijaliwa alama ya "C" katika mtihani wake wa K.S.C.E. Kwa msaada wa Padri Giovani alijiunga na huduma ya utawa ambapo vile vile alijifunza uuguzi pamoja na wenzake kama vile Waithera na Cherotich.

Freda ametumiwa kama mfano wa kutufahamisha kuhusu changamoto ambazo zinawakumba vijana katika uteuzi wa taaluma za kuwawezesha kukidhi mahitaji yao maishani. Wakati mwingine, uteuzi huwa ni wao kwa hiari lakini wakati mwingine huwa ni majaliwa. Kwa mfano, nia yake Freda baada ya kupata gredi ya 'C' katika mtihani wake wa K.C.S.E, ilikuwa ni kufanya kozi katika uhazili, uwekazaji hesabu na kompyuta. Lakini uhaba wa fedha wa kugharamia mafunzo hayo ndio uliositisha azma yake na kumwelekeza kwa Padri Giovani na ombi la kujiunga na utawa. Alipokelewa kwa mikono miwili na kuchukua mafunzo ya utawa pamoja na uuguzi. Tatizo lingine lililomkumba ni la ukosefu mkubwa wa karo baada ya babake kuingilia ulevi wa kupindukia. Ilibidi ategemee msaada kutoka kwa mjomba Mbaabu na Padre Giovani. Jambo hili liliathiri pakubwa mahudhurio yake ya masomo ambapo matokeo yake katika mtihani wake wa K.C.S.E hayakuwa ya kuridhisha.

Tungependa kusema kwamba kutolipa kwa karo ya wanafunzi wakati unaofaa kunaweza kuathiri matokeo yao.Freda na Bob walikuwa ni wanafunzi wenye uwezo kimasomo lakini shida ya karo iliwaathiri na kusababisha matokeo yao duni. Kwa jumla, Freda ni msichana mwadilifu. Pengine msimulizi, Bob ambaye ni kakake hakutaka kutoboa mengi kumhusu dadake hasa kwa kuwa alijiunga na utawa ambapo uadilifu ulihitajika.

Freda alikuwa ni msichana mwenye mapenzi na moyo wa huruma. Wakati wa kulazwa kwake Wairi katika hospitali ya Kenyatta, Freda ndiye aliyegharamia kila kitu kuanzia gari la kumsafirisha Wairi kutoka mjini hadi hospitalini na hata kusimamia gharama ya madawa na matibabu mengine. Hata kifo chake Wairi kilimwathiri sana.Tunamwona kama msichana jasiri. Wakati likizo ilipomalizika na karo kuhitajika hakumwoogopa babake. Alimkabili na kumkumbusha kuhusu karo ambayo ilihitajika na ndipo akawatuma kwa mjomba wao kutafuta usaidizi. Taaluma aliyochagua Freda ilionekana kumfaa, ni kama mwito wake kweli ulikuwa ni wa kumhudumia Mwenyezi Mungu. Bila shaka hana ukabila. Wakati wa hafla ya kufuzu kwake, vijana wote marafiki walihudhuria bila kujali kabila Mfano wake Freda unafaa kuigwa na vijana wa kike katika mazingira haya yenye changamoto nyingi. Uhusika wake una uhalisia kwani kunao wasichana wengi wanaojiunga na usista katika jamii. Uamuzi kama huo huenda ukatokana ama na imani zao au kwa kukosa taaluma wanazozipenda.

### 3.6. Swaleh

Tunaweza kudai kwamba huyu ni mhusika ambaye amechanganya sifa za bapa sugu na mraba mmoja. Njogu na Chimerah (2008 :42) wanamweleza mhusika wa mraba moja kama yule ambaye sifa yake ni moja tu. Hata hivyo hili ni swala la mjadala kwani si kawaida kwa mtu kuwa na sifa moja tu. Licha ya haya, tunasema kwamba sifa moja kuu inayodhihirika zaidi kwa Swaleh ni ya utovu wa maadili kwa sababu anaiba kwa mabavu, analangua madawa ya kulevya na hata kumtafutia kahaba waziri Rashid Hamisi. Alikuwa ni mwanawe Inspekta Fadhili wa kituo cha Polisi cha Bondeni. Yeye kama Wairi alikosa mwongozo bora wa wazazi wake kwa sababu hawakuwa na wakati wa kukaa na mwanao na kumshauri ipasavyo.

Swaleh ametumiwa kama kielezo cha malezi mabaya yaani yanayowapata watoto ambao wazazi wao wanashindwa kutenga muda wa kuwashauri na kuwaelekeza kuhusu hali ya

maisha na kuwaongoza itakikanavyo.Kwa mfano wazazi wake yaani Inspekta Fadhili na mkewe hawakumtengea mwanao wakati wa kumshauri. Tunaelezwa (uk 146) kwamba babake alipotoka kazini alimchukua mkewe wakaelekea mjini kukagua biashara yao ya hoteli mjini nakurudi usiku wakati watoto walishalala. Isitoshe Swaleh alianza kufuta bangi akiwa katika kidato cha pili lakini hakuchukuliwa hatua kwa sababu ya cheo cha babake. Hata masomo hakuyatilia maanani na hatimaye kupata gredi ya chini kabisa (uk 147) alijiunga na genge la majambazi la kuwaibia watu kwa mabavu. Swaleh ni kijana ambaye alikosa maadili kabisa. Licha ya wazazi wa Swaleh kujua mambo hayo hakuna hatua yoyote waliyochukua dhidi yake.

Swaleh ni jambazi sugu. Walizoea kukodesha bunduki kutoka kwa polisi fisadi na kutumia silaha hizo kutekeleza visa vya unyang'anyi wa mabavu. Kifo chake na mwenzake Kariuki kilitokana na tabia hizo wakati jaribio la unyang'anyi lilitibuka na hata wakapoteza bunduki waliyokodesha. Alijihusisha pia na ulanguzi wa madawa ya kulevya. Alikuwa ni wakala wake waziri Rashid Hamisi katika biashara hii haramu ambapo walisambaza madawa ya kulevya kama kokeini katika vyuo vikuu na taasisi nyingine za elimu na hivyo kuchangia pakubwa katika kuharibu vijana katika jamii. Isitoshe hata alitumiwa na waziri huyo kumtafutia wasichana. Hivyo ndivyo alivyompata Wairi na kuanzisha urafiki na waziri huyo. Lakini jinsi ilivyo ni kwamba uhalifu haulipi chochote. Hatimaye alipigwa risasi na polisi waliokuwa wakimsaka kwani tayari alikuwa ni jamabazi sugu aliyekuwa akisakwa na polisi kwa vitendo vingi vya uhalifu ambavyo alivitekeleza.

Hali hii ya Swaleh ni ya kihalisia nchini Kenya kwa sababu kuna tetesi kwamba vijana wengi wanaoshiriki wizi wa kimabavu ni wa umri wa chini ya miaka ishirini na mitano.

### 3.7. Muli

Huyu ni mhusika bapa sugu. Hii ni kwa sababu katika tabia yake tangu utoto hadi kifo chake cha mapema hakuna chochote chanya kinachoelezwa (uk147). Yeye vile vile alikuwa ni

mhasiriwa wa malezi mabaya. Kwa vile hakuwa na baba, aliiga mienendo mibaya kutoka kwa mamake ambaye alikuwa ni malaya. Kwa hivyo alikosa ushauri wa mzazi akajiingiza mapema katika unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya kama kokeini. Hatimaye aliishia hospitali ya wagonjwa wa akili ya Nyayo na hata baada ya kutibiwa na kupona na kuruhusiwa kuondoka baada ya kupona kabisa, tena aliirudia dawa hiyo ambapo sasa ilimvuruga akili kabisa. Kifo chake kilitokea alipombaka mke wa polisi katika kituo cha Polisi cha Bondeni ambapo polisi huyo alimpiga risasi na kumwua papo hapo. Anajitokeza vile vile kama mhusika kinyago ambaye anatumiwa kukejeli jina zuri la vijana. Uhalisia wake umo katika kulelewa na mzazi mmoja huku akikosa kumjua babake. Kuna vijana wengi wanaojikuta katika hali hii siku hizi. Vilevile kuna uhalisia mkubwa katika hali ya Muli kutumia madawa ya kulevya. Hili ni tatizo linaliwakumba vijana wengi nchini Kenya.

### 3.8. Okach

Yeye ni mhusika wa kimapinduzi ambaye amebeba jukumu la kuwahamasisha vijana kuhusu matatizo yanayowakumba katika jamii. Anatumika kama sauti ya vijana wenzake. Ingawa haathiriwi moja kwa moja na matatizo yanayowakumba wenzake, anajitokeza kama sauti horomo ya kutambua matatizo yanayowakumba vijana pamoja na chanzo cha matatizo hayo na masuluhisho yake. Kati ya vijana hawa wa Nyayo, Okach na Jamila ndio waliofaulu kabisa kielimu. Baada ya kumaliza masomo yake ya shule ya upili alifuzu na kujiunga na chuo kikuu kusomea uanasheria. Dhana ya vijana wa Nyayo imetumiwa na Okach kurejelea kizazi ambacho kimezaliwa wakati wa utawala wa rais Moi ambaye falsafa yake ilikuwa ni "Nyayo." Kwa jumla Okach alikuwa na akili pevu na uelewa wa ndani kabisa kuhusu siasa za nchi. Alikuwa ni mshauri mzuri sana. Aliwahi kumtembelea Bob katika shule ya upili yeye akiwa katika chuo kikuu na kumhamasisha kufanya bidii masomoni. Ushauri wake Okach ulimpa Bob ilhamu kubwa ya kusoma kwa bidii.

Wakati wa dhifa yake Freda (uk 138-139) ambapo Okach alijibainisha kama kiongozi wa watoto wa Nyayo. Alionyesha uelewa mkubwa sana kuhusu matatizo ya watoto wa Nyayo ambayo aliyatoa. Baadhi ya matatizo aliyoyatoa ni kama vile malezi ambayo watoto wanakosa kupata kutoka kwa wazazi wao. Hii ni kwasababu kutokana na mishahara duni ambayo wazazi hupata daima wamo mbioni kutafuta mbinu za kuongeza pato na hivyo basi kukosa nafasi ya kuhudumia familia zao. Aligusia pia mfumo wa elimu na ukosefu wa kazi. Aliwashauri vijana kuwatambua maadui zao na kuwa macho, akawahimiza kutokata tamaa, wazifahamu haki zao na kisha washirikiane. Okach alikuwa mshauri mwema wa vijana wenzake. Aliweza kuwapa mawaidha mwafaka kuhusu mwelekeo wao maishani ili wapate ufanisi. Si ajabu kwamba Mwenyezi Mungu alipomjalia Bob utajiri wa ghafla, alimwajiri Okach kama wakili wake wa kumshauri kuhusu mambo ya uwekezaji kwani baada ya masomo yake katika chuo kikuu Okach alifuzu na kuwa mwanasheria.

### 3.9. Konstebo Kerogo

Tunamweleza kama mhusika mjenzi. Kwanza anatusaidia kuelewa mapendeleo yaliyomo katika kitengo cha polisi kuhusiana na kupandishwa vyeo. Pia anachangia pakubwa matatizo yanayowakumba wanawe kwa ajili ya ulevi wake wa kupindukia. Huyu ndiye babake Bob na Freda na mumewe Maria.Alikuwa ni polisi wa cheo cha konstebo katika kituo cha Polisi cha Bondeni. Kwanza ametumiwa kama mfano wa wahasiriwa wa mapendeleo kazini. Yeye ni afisa ambaye ametuama katika cheo kimoja kwa miaka mingi huku akipitwa hata na vijana ambao walijiunga na kikosi hiki baadaye na hata akahusika katika kuwafundisha kazi baadhi yao. Jambo hili lilimfanya akapoteza matumaini na kuingilia ulevi na hivyo kusahau na kupuzilia mbali majukumu yake kama mzazi, hatua ambayo iliathiri pakubwa familia yake upande wa lishe na hata elimu ya watoto wake. Kabla ya kuingilia ulevi alikuwa akiwajibika kwa kumpa mkewe kiasi fulani cha pesa kila mwezi ili kuendeshea nyumba, ingawa kiasi

chenyewe hakikutosha. Labda udhaifu wake mkubwa ulikuwa kwamba hakuthamini kufanya kazi ya ziada kama wenzake ili kujazia pengo la udogo wa mshahara.

Baada ya kukata tamaa Kerogo alibadilika tabia na kawa mlevi mkubwa. Alishindwa kabisa kukidhia familia yake mahitaji yote muhimu huku watoto wake waliokuwa katika shule za upili wakitegemea misaada kutoka kwa watu wengine. Mbali na tabia hii ya ulevi, vilevile alibobea katika uzinzi ambao hatimaye ulichangia kifo chake baada ya kuambukizwa maradhi ya ukimwi. Kutokana na tabia yake tunaona jinsi kutowajibika kwa wazazi kunavyoweza kuathiri watoto kielimu.

### 3.10. Mama Maria

Ni mhusika wa kisaikolojia. Wamitila (2008:387) anamweleza mhusika wa aina hii kama yule ambaye sifa zake zinadhihirisha unyonge na hali ya kukata tamaa kutokana na kudhulumiwa na kudhalilishwa na jamii. Tunamwainisha hivi kutokana na taabu zinazomkumba katika kuwalea wanawe baada ya mume wake kuingilia ulevi na kuyapuuza majukumu yake. Huyu ndiye mkewe Konstebo Kerogo na mama yao Bob na Freda. Umuhimu wake mama huyu ni kwamba ametumiwa kama kielelezo cha mzazi mwema mwenye kuwajibika na kuyajali maslahi ya wanawe na hata mumewe. Mama huyu amesawiriwa kwa sifa kadhaa. Anaonyesha moyo wa simba wa kuhimili matatizo mazito ya kijamii. Mumewe alipoingilia ulevi alisimama imara kuwalea wanawe, wakati mwingine akiomba msaada kutoka kwa nduguye Mbaabu.

Mama Maria alikuwa mcha Mungu na msomaji makini wa Bibilia na asiyekosa kwenda kanisani siku ya Jumapili. Alionyesha nidhamu ya hali ya juu hivi kwamba hata mumewe alipoingilia ulevi wa kupindukia, hakumlaumu bali alisema kwamba binadamu waliishi kulingana na mpango wa Mwenyezi Mungu; akawa anamuombea mumewe kila siku ili

Mungu ambadilishe. Alikuwa ni mlezi mwema ambaye aliwahimiza wanawe kufanya kazi kwa bidii shuleni. Mama huyo alikuwa ni mdadisi wa kuhakikisha kwamba wanawe hawajiingizi katika mambo ya kihalifu. Wakati Bob alikuwa akitafuta stakabadhi za kusafiria Tanzania na Vera, aliwahi kufika nyumbani kwao akiendesha gari kubwa la Vera kutafuta picha. Mama yake alipomwona na gari hilo alishuku kwamba pengine mwanawe ameanza kujiingiza katika uhalifu ndipo akataka kujua asili ya gari hilo. Wazazi wengine labda hawangeshugulika kujua ukweli kama huo. Mama huyu alikuwa na mapenzi ya dhati kwa mumewe. Kwa mfano dhifa ya kusherehekea kufuzu kwa Freda iliingiliana na kulazwa baba yao katika hospitali ya Kenyatta. Badala ya kwenda kwa sherehe, mama huyo alichagua kwenda hospitali na kumwuguza mumewe ambaye hali yake ya afya ilizorota siku hiyo. Wake wengine hawangemjali mume mlevi kama huyo asiyewajibika.

Maria anajitokeza vilevile kama msuluhishi. Kwa mfano, ndoa baina ya Jamila na Bob iliwakera sana wazazi wake Jamila na kwa muda mrefu, hawakutaka kutangamana na familia yake Bob hata kidogo. Lakini kutokana na ushawishi wake mama Bob, hatimaye walisafiana nia na kushirikiana kama familia moja huku Bob akiwasaidia kwa kila hali ya kifedha. Mama huyu anajitokeza kama mtu mnyenyekevu asiyethamini maisha ya kifahari. Mwanawe alipopata utajiri na kuhamia mtaa wa kifahari wa Mlimakuu, awali jitihada zake Bob za kumshawishi mama yake ahamie huko hazikufua dafu huku akidai kwamba tayari alikuwa ameyazoea maisha ya mle misheni. Mama huyo ambaye aliwalea wanawe kwa taabu mwishowe akawa anaishi maisha ya starehe yasiyo na bugudha. Maria ni mhusika bapa sugu na tena msaidizi. Amedumisha msimamo wake kwa uadilifu katika hadithi nzima. Mama Maria anaonyesha uhalisia kwani katika jamii zetu kuna wanaume wengi ambao wameingilia ulevi wa kupindukia na kuwaachia wake zao majukumu ya kulea na kulisha watoto.

### 3.11. Waziri Rashid Hamisi

Huyu ni mhusika mjenzi kwa sababu anasaidia kustawisha sifa zao Swaleh na Wairi kama walanguzi wa madawa ya kulevya na ukahaba mtawalia. Anachangia pakubwa shida zinazowakumba vijana.Yeye alikuwa ni waziri chipukizi akishikilia Wizara ya Ulinzi. Waziri huyu anawakilisha sura mbaya ya Baraza la Mawaziri. Mwandishi, yamkini amemtumia kama kielelezo cha uozo unaopatikana katika Baraza la Mawaziri katika nchi za Kiafrika na uteuzi wa mawaziri ambao hawajiheshimu huku wakionyesha hali ya juu ya utovu wa nidhamu. Waziri Rashid katika uchipukizi wake haitetei hadhi ya vijana. Badala yake anachangia kuzorotesha hata zaidi hali ya vijana wapotofu kama Swaleh.

Isitoshe, Waziri Rashid anajihusisha kimapenzi na wasichana ambao hata tabia zao hazielewi vyema. Kwa mfano siku ya kwanza ya kukutana naye Wairi kupitia kwake Swaleh, alikuwa tayari kufanya mapenzi naye. Hakujali kufanya uchunguzi ambao ungemfaa na angegundua kwamba Wairi alikuwa ni kahaba sugu ambaye hakuchagua wanaume. Bila shaka kama haingekuwa kwa kula kitanzi kwa sababu ya mauaji ya Rita King bila shaka chuma chake kilikuwa motoni na angekufa kutokana na ukimwi ambao tayari ulikuwa ushamchukua mpenzi wake Wairi. Mbali na uzinzi, Waziri Rashid pia analichafua jina zuri la mawaziri kwa kujihusisha na ulanguzi wa madawa ya kulevya huku akiwatumia vijana kama Swaleh kusambaza mihadarati hiyo hata katika vyuo vikuu.

Sifa ya mwisho mbaya ambayo Waziri Rashid anabainisha ni kwamba yeye ni mwuaji. Kwanza alimwua Rita King mwanawe Seneta Humprey King ambaye alikuwa akifanya utafiti nchini Kenya. Alimwua bintiye King baada ya kumbaka. Vilevile ili kuondoa ushahidi wa kumhusisha na mauaji hayo, Waziri Rashid alihakikisha kwamba afisa yule aliyekuwa na ushahidi kuhusu mazungumzo ya simu baina yake na Rita King siku ya kupotea kwake vilevile aliuawa. Waziri huyo ni mhusika kerekecha ambaye ametumiwa kukejeli mawaziri

duni serikalini wanaoharibu sifa ya serikali na nchi. Katika serekali yetu ya Kenya tumekuwa na ripoti katika miaka ya hivi majuzi kuwahusu mawaziri wenye tabia au mienendo potofu ya kutiliwa shaka.Baadhi yao wametajwa bungeni kuhusiana na ulanguzi wa madawa ya kulevya na hata wengine wakadaiwa kuonekana katika barabara ya Koinange usiku wakitafuta makahaba.Hii inathibitisha kwamba uhusika wake Rashid Hamis una uhalisia katika jamii.

### 3.12. Kamash

Yeye ni mhusika kerekecha kwa misingi kwamba vitendo vyake vya kukodisha bunduki yake kwa vijana majambazi vinadhihaki sifa nzuri za kikosi cha polisi. Huyu alikuwa ni afisa wa polisi kutoka kituo cha polisi cha Mjinikati. Afisa huyu bila shaka ametumiwa kama kielelezo cha uozo unaopatikana katika kikosi hicho ambapo baadhi ya Polisi hukodisha bunduki zao kutumiwa katika uhalifu huku wakilipwa kwa kila operrsheni. Kamash aliripotiwa kupata shilingi elfu moja kwa kila operesheni (uk4) Afisa huyo alikuwa na mazoea ya kukodisha bunduki yake kwa kijana Swaleh ili aitumie kutekeleza wizi wa kimabavu. Lakini kwa vile siku za mwizi ni arobaini, kisa cha mwisho ambacho Swaleh na mwenzake Kariuki walijaribu kutekeleza hakikufaulu. Kariuki alitekwa na walinzi wa Mhindi ambaye nyumba yake walinuia kushambulia ili kupora pesa. Bunduki aliyokuwa nayo Swaleh nayo iliponyoka ikaanguka. Bila shaka uchunguzi wa baadaye ungethibitisha nambari za bunduki hiyo na afisa aliyeimiliki pamoja na kituo cha polisi ilipotokea. Hayo yangemtia Kamash matatani. Swaleh aliuawa siku chache tu baada ya kisa hiki. Ni polisi kama Kamash wanaoliaribu jina zuri la kitengo hicho na hata kuwaingiza vijana wakembe katika uhalifu. Maafisa wa aina hii wanapatikana katika kikosi cha polisi.

## 3.13. Seneta King

Kwa vile upelelezi wa majasusi wale wa FBI ambao Seneta King aliwahusisha katika kuchunguza mwuaji wa bintiye ulifichua mengi kuhusu watu wa Kenya pamoja na serikali kwa jumla, itafaa kumchambua japo kwa kifupi, seneta huyu wa Marekani. Mwandishi alimtumia kuonyesha uozo na ufisadi uliojaa katika nchi yetu pamoja na ukosefu wa uwajibikaji, uwazi na uangavu miongoni mwa maafisa wa serikali. Kwa jumla seneta King alikuwa na mapenzi ya dhati kwa mwanawe wa pekee Rita King. Jambo hili linadhihirishwa na juhudi alizofanya kuhakikisha kwamba mwuaji wa mwanawe amepatikana. Kwanza alihusisha serikali yake baada ya kugundua kwamba uchunguzi wa humu nchini haungefua dafu kwa sababu ya ufisadi uliokithiri. Kwa hivyo maafisa majasusi wa shirika maarufu la FBI, walihusishwa.

Jambo lingine ni kwamba seneta King alikuwa tayari kutoa zawadi nono ya dola milioni moja sawa na shilingi milioni sabini (katika ubadilishaji wa fedha wa wakati huo) ili kuhakikisha kwamba mwuaji wa mwanawe amepatikana.Uchunguzi huo ulibainisha mambo fulani kuhusu nchi ya Kenya. La kwanza ni kwamba watu wa Kenya hawakuwa waaminifu. Hili lilitokea wakati kituo cha kupokea ushahidi au habari zozote muhimu kutokana na kifo cha Rita King kilifunguliwa huku shilingi mia tano zilizotolewa kwa kila shahidi. Ikabainika kwamba ushahidi wote ulikuwa wa bandia tu. Wote waliofika pale walikuwa na lengo la kujifaidi tu kutokana na fedha hizo. Jambo lingine lililodhirika ni kwamba serikali ya Kenya haikutaka ukweli wowote ujulikane. Kila juhudi ilifanywa kumfunika waziri huyo mwuaji. Hata vyombo vya habari vilivyomilikiwa na serikali vilijaribu kuikashifu serikali ya Marekani kwa kuchafua sifa za taifa la Kenya. Lakini ukweli uliibuka wakati Bob alipoutoa ushahidi wake usiopingika.Seneta King ni mhusika msaidizi ambaye amechangia kuyabadili maisha yake Bob kwani zawadi aliyoitoa ndiyo ilileta mapinduzi ya kiuchumi maishani mwake kijana huyo. Kuhusu uchunguzi wa Seneta King kuhusiana na mauaji ya mwanawe,

jambo hili lina uhalisia mkubwa. Miaka ya tisini, kulikuwa na mwanamke mzungu aliyeitwa Julie Ward aliyeuawa nchini Kenya. Ilimbidi babake atumie polisi wa Scotland Yard kufanya upelelezi kuhusu mauaji ya bintiye.

### 3.14. Mjomba Mbaabu

Yeye ni mhusika msaidizi ambaye alikuwa na uhusiano wa karibu na Bob kama mjomba wake. Kupitia uhusiano huu tunaelewa matatizo aliyoyapitia Bob hadi kufikia kilele cha ufanisi na hata kuishi mtaa mmoja wa kifahari na huyo mjomba wake. Huyu aliyekuwa mjombake Bob pia alikuwa afisa mkuu wa benki akiishi mtaa wa kifahari wa Mlimakuu. Ametumiwa kama mhusika mjenzi au msaidizi ambaye alitoa mchango katika elimu yake Bob. Huyu ni mtu mwadilifu ambaye amemwoa mke mwenye roho ya nyoka. Mama Kegonda ni mtu mwenye chuki na bahili, hali inayotuonyesha jinsi wanaume wazuri huwaoa wanawake ibilisi na vivyo hivyo wanawake wazuri kuolewa na wanaume ovyo kama ilivyokuwa kwake mama Maria na mumewe Konstebo Kerogo. Kwa jumla mjomba Mbaabu alikuwa ni mtu mkarimu. Mbali na kuwasaidia watoto wa dadake kwa ulipaji wa karo vilevile alisaidia sana huyo dadake mara kwa mara katika lishe ya watoto wake. Aliweza vilevile kumtafutia Bob kibarua kwa Bw. Devji rafiki yake wa Kihindi. Isitoshe wakati wa likizo Bob aliweza kumsaidia mwanawe Kegonda na masomo ya ziada. Hatimaye, Bob alipojaliwa utajiri waliweza kushirikiana katika biashara kama vile ununuzi wa Safari Hotel.

### 3.15. Devji

Ni mhusika msaidizi.Anachangia maudhui ya dhuluma ambazo vijana hupata kutoka kwa waajiri wao . Huyu alikuwa ni mfanyibiashara Mhindi, rafiki yake Mbaabu. Aliwahi kumpa Bob kibarua kutokana na ombi lake Mbaabu. Jambo moja linalobainika kutokana na tabia zake Devji ni kwamba, kwanza yeye ni bahili. Bob alifanya kazi zote nzito lakini akamlipa shilingi mia mbili tu mwishoni mwa siku. Pia hakuwa tayari kumpa ajira ya kudumu kwa vile

kazi zote muhimu zilishikiliwa na familia. Kunao uhalisia mkubwa katika uhusika wake kwa sababu waajiri wengi wakihindi hupendelea kuwaajiri wafanyikazi katika viwanda vyao kama vibarua na kwa mishahara duni.

### 3.16. Mama Kegonda

Ni mhusika mjenzi. Kutokana na roho yake mbaya tunafahamu dhiki ambazo Bob alipitia kwa sababu mama huyo hapo awali alikuwa ni mwenye taadi na inda. Huyu ni mkewe Mbaabu mjombake Bob. Kwa jumla mwanamke huyu ana roho ya nyoka. Hakutaka kamwe mumewe asaidie familia ya dadake. Siku Bob na Freda walitumwa na mama yao kutafuta msaada wa karo alitoroka sebuleni mara tu watoto hao walipoingia. Vilevile hapo awali hakuwa amejua kuendesha gari lakini alipomwoona mumewe akimtuma Bob na gari lao mjini kununua vitu, aliudhika hadi akajifundisha kuendesha gari mwenyewe. Inashangaza kwamba mwishowe baada ya Bob kuwa tajiri, tabia yake ilibadilika hata wakawa na uhusiano mzuri. Huenda mabadiliko haya yalikuwa ya kinafiki. Kunao uhalisia katika tabia yake kwa sababu kunao watu fulani ambao wataonyesha madharau kwa wengine lakini Mungu anapowainua wale waliowadharau wanageuka na kuanza kuwaheshimu

### 3.17 Mwalimu Ramadhani na Mkewe

Hawa ni wahusika wajenzi ambao wanachangia maudhui ya malezi na hasa matatizo yanayowakumba vijana kutokana na malezi ya kudhibitiwa. Hawa ni wazazi wake Jamila. Wote walikuwa ni walimu katika shule ya msingi ya Uhuru, huku Ramdahan akiwa ndiye mwalimu mkuu naye mkewe akifundisha hisabati katika shule iyo hiyo.Wametumiwa kama kielelezo cha wazazi wakali na waangalifu, ambao huwalea wanao kwa udhibiti mkali na masharti bila kuelewa kwamba watoto hao wanapotangamana na wenzao katika taasisi za elimu huenda wasizingatie mawaidha ya wazazi wao kulingana na uhalisia wa mazingira.

Wakiwa waislamu wenye itikadi kali walimlea mwanao Jamila kwa uangalifu mkubwa huku wakimshauri kutosuhubiana na watu wasiokuwa waislamu lakini kinyume na matarajio yao kilitendeka. Jamila hakuolewa tu na mtu ambaye hakuwa mwiislamu bali pia aliupoteza ubikira wake hata kabla ya kuolewa akiwa katika kidato cha pili. Ndoa yake awali iliwaudhi mno wazazi wake lakini wakasalimu amri walipogundua kwamba hawangebadili msimamo au uamuzi wa binti yao. Wanasahau kwamba mbinu zile za zamani za kuwadhibiti watoto wao hazifui dafu na zimepitwa na wakati. Japo wazazi wa aina hii wangali wapo, vijana siku hizi wana njia nyingi za mitagusano. Si rahisi sana kwa wazazi kuwashawishi kuhusu ndoa. Wazazi wake Jamila walichangia bila kujua kuharibika kwa binti yao. Kwa kumdhibiti walidhani kwamba angebaki "safi ." lakini kinyume na matarajio yao walichangia kumpa mwanao hamu ya kuwajua wanaume. Wazazi wa aina hii wamo katika jamii yetuhasa zile hafidhina na kwa hivyo wana uhalisia.

**3.18. Inspekta Fadhili na Mkewe/ Sajini Njoroge na Mkewe**

Hawa vile vile ni wahusika wajenzi kwa sababu wanachangia kuharibika kwa wanao Swaleh na Wairi mtawalia. Tumechagua kuziweka pamoja familia hizi kwa sababu sifa zao zinafanana. Inspekta Fadhili ni babake Swaleh naye Sajini Njoroge akiwa ni babake Wairi. Kinachozifananisha familia hizi ni kwamba wazazi hao hawakupata nafasi ya kuwaelekeza wanao. Wote, baada ya kazi zao rasmi, walifululiza kushughulikia biashara zao binafsi ili kuongezea pato. Matokeo yake yalikuwa kwamba wanao, Swaleh na Wairi waliharibika na kuwa jambazi na kahaba mtawalia. Wazazi hawa wanaendeleza maudhui ya matatizo ya ulezi pamoja na ukosefu wa uwajibikaji miongoni mwa wazazi.Swaleh kwa mfano anaharibika kwa sababu ya ulegevu wa babake ambaye ni polisi wa ngazi ya juu kazini. Ni jambo la kinaya kwamba mwanawe askari wa kiwango cha inspekta anakuwa ni mhalifu sugu. Badala ya kubatili udongo ungali maji katika kidato cha pili wakati mwanawe alipoanza uhalifu wa kutumia madawa ya kulevya, Inspekta Fadhili alimdekeza na kumfunika.

Swaleh baadaye alijihusisha na uhalifu ukiwemo wizi wa mabavu na ulanguzi wa madawa ya kulevya, na hata ulevi wa kupindukia. Kujihusisha kwake na unyang'anyi ndiko kulikosababisha kifo chake hatimaye. Wairi naye vivyo hivyo kwa sababu ya kukosa ushauri wa wazazi alijiingiza katika uzinzi mapema. Akiwa katika kidato cha pili alikuwa mjamzito baada ya kutiwa mimba na mwalimu mkuu wa shule yake Bw. Nyamboki. Baada ya kujifungua na mtoto kufikia umri wa kumwachia mamake. Wairi alijitumbukiza katika ukahaba ambao ulimletea maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi na hatimaye kifo. Wahusika hawa wana uhalisia kwa sababu wazazi wengi katika jamii wamo mbioni kutafuta pesa huku wakisahau majukumu yao mengine muhimu.

### 3.19 Mwalimu Nyamboki

Tunamwainisha kama mhusika kerekecha kwa sababu hali yake ya kufanya mapenzi na wanafunzi wake kama mwalimu mkuu inatoa taswira mbaya sana ya taaluma ya ualimu. Mwalimu mkuu anatakiwa kuwa kielelezo si kwa wanafunzi tu bali pia kwa walimu wale anaowasimamia. Basi ikiwa yeye ndiye anayeonyesha mfano mbaya kama huo walimu chipukizi watafanyaje? Ni mfano upi watakaoiga? Kuna walimu wengi wenye tabia hii ya uzinzi katika jamii yetu kwa hivyo mwalimu Nyamboki ana uhalisia kwani walimu kama hawa wanaosababisha matatizo kwa vijana wamewakilishwa naye.

### 3.20. Hitimisho

Kunao wahusika wengine ambao hatukuweza kuwashughulikia kama vile Achieng, Kajuju, Kariuki, mamake Muli na Mwaora; lakini tunaamini kwamba wale ambao tumechunguza wanatosheleza madhumuni ya tasnifu hii. Hii ni kwa sababu vijana kama Achien'g na Kajuju na hasa matatizo yao tayari wameangaziwa katika uhusika wa wenzao kama vile Jamila, Freda na Wairi. Wahusika ndio uti wa mgongo na uhai wa kazi yoyote ile ya fasihi. Usawiri mwafaka wa wahusika ndio huipa ufanisi kazi husika ya fasihi. Kutimizwa kwa dhamira

pamoja na maudhui hutegemea uhalisia ambao msanii anawapa wahusika wake. Katika tasnifu hii tumegundua matatizo mengi ambayo yanawakumba vijana pamoja na muonoulimwengu wa vijana wenyewe.

Jambo moja muhimu ambalo linadhihirika katika uhusiano wa vijana hawa ni kwamba hawana ukabila. Wakiwa na hafla, wote wanahudhuria bila kubaguana. Vilevile wakiwa katika maombolezo, wote tena wanahudhuria. Hii ndiyo taswira halisi ya vijana katika misingi ya nadharia ya uhalisia inayotuongoza katika tasnifu hii. Tukimalizia, tungependa kusema kwamba wahusika wote katika riwaya hii wana uhalisia kwa sababu matendo yao yana shabihiana na ya bvijana wa kawaida katika jamii. Hata hivyo ingawa tumewarejelea wahusika katika makundi tofauti tofauti ya uainishaji katika kuwahakiki, ukweli ni kwamba katika misingi ya uhalisia, wahusika wenye uhalisia hubeba sifa changamano za kuwafanya wafanane na binadamu wa kawaida.

## SURA YA NNE

## UHAKIKI WA MAUDHUI KUHUSU VIJANA

### 4.0. Utangulizi

Katika sura hii tumejadili swala la maudhui. Wamilitila (2003) anaelezea maudhui kama jumla ya mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Naye Mbatiah (2001) anaelezea maudhui kama jumla ya mawazo, fikira, dhamira na hisia zinazowasilishwa na kazi ya kifasihi. Anaendelea kusema kwamba maudhui yanajibu swala la "nini" kazi ya fasihi inazungumzia. Maudhui vilevile yanaweza kuchukuliwa kama ujumbe au mafunzo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi. Katika sura hii sehemu kubwa ya maudhui inahusu uhakiki wa hali ya vijana kwa kina na matatizo nyeti ambayo yanawakumba katika jamii pamoja na chanzo cha shida zenyewe. Mbali na maudhui haya hasi yanayowahusu vijana kunayo mengine chanya ambayo tumeyazungumzia.

### 4.1. Ukosefu wa Malezi Bora

Familia ni asasi muhimu sana katika malezi ya watoto. Pale ambapo kuna uthabiti katika asasi hii basi watoto watapata maelezo na mwongozo bora lakini pale ambapo kuna utepetevu basi majukumu muhimu yatapuuzwa na watoto hawatapata mwelekeo bora. Kimsingi, familia imefungamana na asasi ya ndoa ambayo inaaminika kuasisiwa naye Mwenyezi Mungu wakati alipowaumba binadamu wa kwanza, yaani Adamu na Hawa, haya ni kulingana na Biblia. Ni katika asasi hii ya ndoa na kisha familia ambapo watoto basi wanatarajiwa kupata malezi yanayofaa. Malezi ni mchakato changamano sana ambao unajumuisha mambo kadha yakiwa pamoja na lishe, mavazi, makao, elimu pamoja na ushauri ambao ni mwafaka. Tukizungumzia asasi ya ndoa na kisha familia tunachukulia kwamba familia kamili itakuwa na baba, mama kisha watoto watakaozaliwa. Ni katika mazingira haya kamili ambapo watoto wanatarajiwa kupata malezi bora. Mbali na mambo yale ya kimsingi ambayo tumedai yanajumuisha malezi bora, hata urithi kwa mtoto ni jambo ambalo linampa mtoto huyo

msingi thabiti wa kuyajengea masiha yake. Hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kwamba asasi hii imekumbwa na misukosuko anuwai hivi kwamba uthabiti ambao unahitajika ili kuwezesha malezi bora haupo tena. Basi kuna matatizo mengi yanayowakumba vijana na ambayo yamehusiana na asasi ya ndoa au familia. Baadhi ya matatizo yanaathiri vijana bila kujali jinsia ilhali mengine yanawatatiza vijana kutegemea jinsia zao.

Tatizo la kwanza ambalo vijana wanakumbwa nalo linahusiana na kuzaliwa nje ya ndoa ambapo wakati fulani kijana kama huyo asijue babake mzazi. Katika mazingira ya aina hiyo iwapo kijana huyo ni wa kiume, atataka kumjua babake mzazi ni nani na iwapo mamake hamweelezi ukweli unaofaa, basi kijana kama huyo ataachwa na maswali mengi sana akilini mwake ambayo yatamwaathiri kisaikolojia, hata kuweza kumsukuma katika tabia zingine mbovu ambazo hazifai. Isitoshe, mazingira ambamo kijana kama huyo ambaye hana baba huzaliwa yanaweza kumwaathiri vibaya kitabia. Tuchukulie hali ambapo kijana kama huyo ambaye mamake mzazi ni kahaba, mtoto kama huyu anapobalehe mama mzazi hawezi kumpa mwongozo bora ambapo kuna hatari kwake kuingilia mienendo mibovu isiyofaa na hatimaye akapotoka maishani mwake. Vilevile kuna tatizo la kujitambua ambapo kijana wa aina hiyo hataweza kujitambua ipasavyo hasa kuhusiana na babake mzazi pale anapoulizwa na wenzake kuhusu babake.

Tatizo lingine linalowakumba vijana na ambalo linahusiana na asasi yenyewe ya ndoa ni kuvunjika kwa ndoa hizo. Katika asasi zote za kijamii ambazo zinamhusu binadamu, asasi ya ndoa ni miongoni mwa zile ambazo zimekumbwa sana na ukosefu wa uthabiti. Kuna visa vingi sana vya kuvunjika kwa ndoa hizi ambapo jambo hilo linapotokea wakati vijana wenyewe wakiingia umri wa kubalehe wanaanza kuitilia shaka asasi hiyo na hata kuichukia. Hata pale ambapo wazazi wanaishi pamoja , ukosefu wa uwajibikaji miongoni mwa mmoja wa wazazi wale unaweza kuathiri sana hali ya watoto hao. Kwa mfano mzazi yule ambaye

anabeba jukumu la kukidhi mahitaji ya familia anapoyapuuza majukumu yake kwa kuingilia ulevi na ukware basi familia itaumia sana kwa sababu mbali na kushindwa kugharamia mahitaji ya kimsingi kama chakula, huenda hata akashindwa kulipa karo na hivyo kuvuruga elimu ya watoto wanaohusika. Jambo kama hilo likifanyika wakati vijana hao wanaingia katika kiwango muhimu cha awamu ya elimu yao kama vile shule ya upili na kisha karo ikosekane, elimu yao itaathirika sana kwa njia hizi.

Matatizo ya kiuchumi vilevile yanachangia hali ya wazazi kutopata nafasi ya kutosha kukaa na wanao na kuwashauri. Hii ina maana kwamba hata pale ambapo wazazi hao wameajiriwa katika huduma za umma, kwa sababu ya malipo au mshahara duni katika ajira kama hizo, wazazi hao wanaporejea nyumbani hulazimika kufululiza hadi kule wanakoendesha shughuli za kuleta mapato ya ziada. Ratiba kama hizi huwanyima kabisa nafasi tosha ya kuwawezesha kukaa na watoto kwa ushauri zaidi na kuwapa mwongozo. Ukosefu wa nafasi ya mtagusano unaofaa kati ya wazazi na wanao vilevile unasababishwa na mfumo wa elimu nchini ambao unatilia maanani sana ufanisi katika mtihani. Jambo hili linaleta ushindani mkubwa kati ya taasisi za elimu nchini huko kila mojawapo iking'ang'ania kuoredheshwa miongoni mwa zile bora na kutangazwa na vyombo vya habari ili umaarufu wake ujulikane na ndipo wavutie wasomi zaidi kujiunga navyo. Katika hali hii watoto hupitisha wakati wao mwingi shuleni, hata wakati wa wikendi na likizoni, kwa mafunzo ya ziada ambapo wanapata nafasi haba ya kukaa na wazazi wao ili wafunzwe maadili. Hii ni sababu kubwa sana inayochangia kuzorota kwa maadili miongoni mwa vijana.

Matatizo hayo yameangaziwa katika *Vipanya Vya Maabara* . Swaleh, Wairi, Muli, Bob, Freda na Jamila ni wahasiriwa wa baadhi ya matatizo ya malezi ambayo tumeyaangazia. Kwa mfano Bob na dadake walikuwa ni vijana wenye uwezo mkubwa kimasomo ambapo wakati mmoja, Bob aliwahi kushikilia nafasi ya pili katika darasa lake akiwa darasa la nne. Isitoshe

akiwa shule ya upili alikuwa amelenga kujitahidi masomoni angalau afuzu vyema ili afanye taaluma ya Uanasheria kama rafiki yake Okach. Hata ilhamu ya kusoma alikuwa nayo huku akipenda kuingia maktabani na kusoma kwa mapana. Lakini kiwango chake cha elimu pamoja na hata cha dadake kiliathirika sana wakati baba yao aliingilia ulevi wa kupindukia na kutupilia mbali majukumu ya ulipaji karo. Katika hali hii vijana hao wakawa wanafukuzwa mara kwa mara kutoka shuleni kwa sababu ya ukosefu wa karo. Matokeo yalikuwa kwamba hawakuweza kufanya vyema katika mitihani yao ya kitaifa na hatimaye wakapata gredi wastani ya 'C' katika mtihani wa K.C.S.E ambayo haingewazesha kujiunga na taasisi za juu kwa kozi mwafaka.

Wairi na Swaleh nao waliathirika kitabia kwa sababu ya wazazi wao kutopata nafasi ya kukaa nao na kuwashauri. Badala yake wazazi wao walitumia nafsi waliyokuwa nayo jioni baada ya kutoka kwenye kazi zao rasmi, kushughulikia biashara zao za kibinafsi ile kujiongezea pato. Hivyo basi wanao wakakosa mtagusano bora wa wazazi. Jambo hilo liliathiri pakubwa sana vijana hao. Wairi alijiingiza mapema sana katika shughuli za mapenzi, hivi kwamba akiwa katika kidato cha pili, tayari alikuwa ni mjamzito baada ya kutiwa miimba na mwalimu mkuu wa shule ya upili alikosomea. Swaleh naye kwa ajili ya tatizo hilo lilo la kutoelekezwa na wazazi wake aliishia kuingilia matumizi ya madawa ya kulevya akiwa katika kidato cha pili huku makosa yake yakifichwa kwa sababu babake alikuwa ni afisa mkuu katika kitengo cha Polisi. Lakini kufichwa kwa makosa yake hakukumsaidia kwa sababu mbali na kutofanya vyema katika mtihani wake wa kitaifa alipofika kidato cha nne hatimaye aliingilia maisha ya uhalifu ukiwa pamoja na wizi wa kimabavu kwa kutumia bunduki iliyokodiwa pamoja na ulevi na ulanguzi wa madawa ya kulevya. Hatima ya maisha hayo ya uhalifu ilikuwa ni kifo chake kwa kupigwa risasi.

Wairi naye vilevile uzinzi wake ulimwelekeza katika ukahaba wa kulipwa katika danguro moja jijini Nairobi, mbali na elimu yake kukatizwa. Kutokana na ngono yake hipo hatari, aliambukizwa maradhi ya ukimwi ambayo yalisababisha kifo chake.Mhasiriwa mwingine wa malezi mabaya alikuwa ni Muli ambaye mamake alikuwa ni kahaba katika kituo cha Polisi cha Bondeni alikoishi na kuendesha biashara katika kantini. Huku akiwa hata hamjui babake, Muli alikuwa katika mazingira ya ukahaba huku akikosa mwongozo bora wa baba mzazi na ndipo akaiga nyendo hizo mbovu mapema maishani mwake kwa kuingilia matumizi ya madawa ya kulevya yaliyoivuruga akili yake hadi akaishia hospitali ya ugonjwa wa akili ya Nyayo. Mbali na umalaya wa mama, Muli alikuwa pia mlevi wa kupindukia. Alijifunza tabia hiyo mbaya kutoka kwa mamake....... (uk 165) na hata baada ya kutibiwa huko na kuweza kupata nafuu, aliirudia tabia hiyo ya matumizi ya madawa ya kulevya. Mwishowe alimbaka mke wa askari polisi ambaye alimpiga risasi na kumwua.

Jambo lingine linalolofungamana na malezi na linaloathiri vijana vilevile linatokana na jitihadi za wazazi wengine wenye itikadi kali ambao hujaribu kuwalea wanao kwa masharti makali wakidhani kwamba huu ndio mwongozo bora ambao wanao wanastahili. Lakini kinyume ni kwamba huu udhibiti ambao hulenga kuhakikisha kwamba wanao hubaki 'safi' badala yake huwajaza na ilhamu ya kutaka kujua ni yapi hayo ambayo wazazi wao wanajaribu kuwazuia wasiyajue. Jamila vilevile alikuwa ni mhasiriwa wa malezi yasiyofaa. Wazazi wake ambao walikuwa ni walimu wenye imani ya dini ya kiislamu walimlea mwanao kwa uangalifu mkubwa sana wasitake asuhubiane na watu wasiokuwa wa dini yake. Bila shaka udhibiti wote na uangalifu mwingi ulimpa Jamila ilhamu ya kugundua na ndipo akaupoteza ubikira wake nyumbani kwao katika chumba ambacho wazazi wake waliamini kilikuwa salama kwake na hata mwishowe akaolewa na kijana yuyo huyo Bob, aliyembikiri na ambaye hakuwa hata mwiislamu. Upinzani wa wazazi wake kuhusu nikahi hiyo haukufua dafu na hatimaye wakasalimu amri.

Kutokana na yote haya ni wazi kwetu kwamba malezi yasiyofaa yanachangia sana matatizo yanayowakumba vijana katika jamii na hata kusababisha kungamia kwa baadhi yao kutokana na vifo vya mapema. Zamani wakati wa kuthaminiwa kwa utamaduni wa mwafrika, malezi ya watoto yalikuwa ni jukumu la jamii nzima ambapo jamii hiyo haingekaa kitako na kumwona mtoto au kijana akiharibika katika jamii bila kuchukua hatua. Tatizo hili, kutokana na maelezo ambayo yametolewa, linawaathiri vijana wa kike na wa kiume.

**4.2. Matatizo ya Madawa ya Kulevya**

Matumizi ya madawa ya kulevya ni tatizo sugu sana ambalo linawaathiri vijana wetu kwa wakati huu. Hivi majuzi kumekuwa na kisa katika Kaunti ya Muranga kuhusiana na matumizi ya pombe haramu iitwayo "The Warrior" ambayo ilisababisha vifo vya vijana wanne na kuwaacha wengine wengi wakiwa vipofu. Na hii haikuwa mara ya kwanza kwa kisa kama hiki kuripotiwa. Isitoshe, mwezi uu huu wa Agosti 2012, kumekuwa na zoezi la kuajiri makruta wa kujiunga na Jeshi la Kenya lakini jambo la kusikitisha ni kwamba iliripotiwa kuwa wengi wa vijana waliofika kwa zoezi hili walikuwa walevi sana yamkini kutokana na uraibu wao kwa vileo hivyo ambavyo aghalabu huwa ni haramu. Katika tasnifu hii, tulivijumuisha vinywaji hivi miongoni mwa madawa ya kulevya ambayo matumizi yake yamekithiri miongoni mwa vijana.

Madawa ya kulevya yanaweza kuelezwa kama kitu chochote kiwe ni cha kunywewa, kuvutwa, kutafunwa au kujidunga na binadamu na ambacho kina uwezo wa kugeuza na kuathiri hali ya kawaida ya utendaji kazi wa mwili wa binadamu. Kisaikolojia, madawa ya kulevya ni kitu chochote ambacho mtu akikitumia ama kwa kukila, kunywa, kuvuta au kudunga kwa sindano huweza kubadili hulka, fikira, tabia au vitendo vyake mtumiaji wa vitu hivyo. Aghalabu matumizi kama hayo huwa ni ya kukusudia kwa madhumuni maalumu aliyo nayo yule anayoyatumia. Vileo hivi vinaweza kugawanywa katika makundi matatu makuu,

yaani, pombe, tumbaku na madawa. Watu wengi hawachukulii pombe na tumbaku kama ni hatari lakini, dhana hiyo si kweli kwani vitu hivyo huweza kugeuka na kuwa hatari sana kwa mtu anapopata uraibu wake. Baadhi ya vinywaji hivi hutegenezwa katika mazingara chafu sana na hata baadhi ya viungo ambavyo vinatumiwa kutengeneza pombe hizi ni kemikali zinaweza kudhuru afya ya binadamu. Vileo hivi huwa havipitii mikononi mwa shirika ambalo linahusiano na ukadiriaji wa ubora wa vinywaji na ufaafu kwa matumizi ya binadamu na ndipo baadhi ya vinywaji vyenyewe vimesababisha vifo na hata kupofuka kwa baadhi ya watumiaji wake. Vingine vimedaiwa kuathiri nguvu za kiume za vijana wengi. Kuna ithibati kwa jambo hili kwa sababu kumekuwa na maandamano katika Kaunti hiyo tuliyoitaja yakiongozwa na wanawake waliodai kwamba waume zao walikuwa wameshindwa kutekeleza majukumu yao ya nyumbani kama wanaume.

Madawa ya kulevya, kando na pombe huwa ni madawa ambayo yanafaa kutolewa kwa ushauri wa daktari kwa ajili ya matibabu ya magonjwa fulani, lakini mara nyingi kwa ajili ya matatizo mbalimbali yanayowakumba watu, matumizi ambayo hayazingatii ushauri wa daktari yamekithiri siku hizi. Madawa ya kulevya yanaweza kuwa ya kiasili yaani yaliyotengenezwa kutokana na mimea kama vile 'kokeni' au 'heroini' au yawe yanayotegenezwa katika maabara kutokana na kemikali kama vile 'L.S.D'; (Lysergic Acid Diethylamide), 'Ecstacy' na 'speed' ambayo yakitumiwa huwa na athari ya kuleta msisimko mwilini mwa mtumiaji na hata kumtia katika hali ya kinjozi na mzubao. Lengo la kuyabuni madawa hayo huwa ni la kimatibabu lakini binadamu ndiye huyageuza na kuyafanya kuwa ni ya kustarehe. Basi mabadiliko hayo ya kimatumizi yakichukua mwelekeo huu mpya yanakuwa sasa ni madawa ya kulevya ambapo viwanda ambavyo vinahusika na utengenezaji wake huwa sasa havitengenezi madawa hayo kwa ajili ya tiba bali ni kwa kutosheleza soko la matumizi ya kujisterehesha.

Madawa ya kulevya huathiri hisia za mtumiaji mpaka akajisahau asielewe alifanyalo. Wacheza sinema ambao hukubali kucheza sehemu fulani za filamu hizo wakiwa uchi, mara nyingi huwa wametumia madawa ya kulevya kama L.S.D. Isitoshe watu wengine wamelipwa ili kulangua baadhi ya vidonge vya madawa hayo katika masoko ya kimataifa kwa kuyameza na kuyabeba matumboni mwao. Kuna mambo mengi ambayo yanachangia matumizi ya madawa hayo. Kwanza kabisa ni athari za makundi fulani katika jamii . Iwapo vijana wakembe wanakuwa na mtagusano na wenzao ambao tayari wamo katika matumizi ya madawa hayo ya kulevya wanaweza kushinikizwa kuyatumia madawa kama hayo. Katika sehemu za mijini na hata mwambao mwa Kenya, baadhi ya vijana wetu wameathirika katokana na utangamano wao na watalii na wageni kutoka sehemu zingine za ulimwengu ambapo matumizi ya madawa haya yamekithiri.

Jambo la pili ambalo limechangia sana matumizi haya ya madawa ni ukosefu wa ajira ambao huwaacha vijana wengi katika hali ya uvivu. Ili kujiondoshea mawazo mengi kuhusiana na matatizo ya kiuchumi yanayowakabili katika jamii vijana wengi wasio na ajira huingilia matumizi ya madawa haya ili kuzisahau shida zinazowakumba. Inadaiwa kwamba wengine huyatumia madawa ili kupata ujasiri wa kuwawezesha kushiriki katika uhalifu bila uoga. Isitoshe inadaiwa kwamba baadhi ya wasanii kama vile wanamziki na wacheza filamu huyatumia madawa hayo ya kulevya kwa sababu tofautitofauti. Kuna wale watakayoyatumia kwa lengo la kupata ujasiri wa kukabili umati katika ukumbi wa kustarehe au kujipunguzia usingizi ili waweze kustarehesha watu kwa vipindi virefu zaidi. Miongoni mwa vijana siku hizi kuna dawa ya kulevya ya "unga unga" inayouzwa madukani kwa bei nafuu. Dawa hii yenye asili ya Bara Hindi huitwa 'kuber; na vijana wanaweza kuimumunya bila kutambuliwa hata wakiwa darasani.

Katika taifa letu la Kenya tatizo la madawa ya kulevya ni la kweli kwani kumekuwa na tuhuma kwamba baadhi ya viongozi mashuhuri nchini wanajihusisha na ulanguzi wa madawa hayo na hata kukawa na Tume ya kuwachunguza baadhi yao mwaka wa 2010. Tatizo hili la madawa ya kulevya limeangaziwa katika *Vipanya Vya Maabara* huku vijana na hata viongozi wakihusishwa na ulanguzi wa madawa haya. Mhasiriwa mkubwa wa madawa hayo alikuwa ni Muli ambaye kwa ajili ya kukosa mwelekezi katika familia aliingilia matumizi ya madawa kama kokeni akiwa na umri mdogo sana. Madawa hayo yaliamwathiri akili hadi akaishia hospitali ya wagonjwa wa akili ya Nyayo ambapo alitibiwa na kupona lakini akarudia tena na hali yake iliivurugika na kuwa mbaya sana kuliko hapo awali. Alipuuza ushauri wa daktari kuhusiana na umuhimu wa kutoyarudia madawa hayo kwani hali yake ingekuwa mbaya kuliko hapo awali. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwani akiwa katika hali hiyo ya kulewa ndipo alipombaka mke wa polisi katika kituo cha Polisi cha Bondeni, kitendo ambacho kilisababisha kifo chake baada ya mume wa mwanamke huyo kumpiga risasi.

Swaleh, ambaye babake alikuwa ni Inspekta wa polisi ni mhasiriwa mwingine wa madawa hayo. Yeye pia kwa kukosa mwongozo wa wazazi aliingilia matumizi ya madawa hayo ya kulevya akiwa katika kidato cha pili. Lakini babake badala ya kuchukua hatua ya kumrekebisha aliyaficha makosa yake. Baadaye maishani akawa ni mwizi wa mabavu. Isitoshe alitumiwa na waziri Rashid Hamisi kama wakala wa kumsambazia madawa ya kulevya katika vyuo vikuu na pia vituo vingine vya kustarehe vilivyopendwa na vijana wa watu matajiri. (uk 113) ……… *mimi ni wakala wake wa kusambaza mihadarati. Nimemfanyia kazi hiyo kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa* ………Kuhusishwa kwake waziri Rashid Hamisi katika ulanguzi wa madawa haya hasa kwa kuwatumia vijana kama wakala wa kumweendeshea biashara hii haramu ni jambo la kuaibisha kwa sababu viongozi kama yeye wana jukumu la kuyalinda maslahi ya wananchi na kuhakikishia afya ya vijana wa taifa hilo kwani ndio tegemeo la nchi hiyo kwa siku zijazo. Ikiwa basi viongozi ambao wanatarajiwa

kuweka mazingira salama ndio tena wanaohusika katika kuyavuruga basi hii ni hali ya kinaya katika uongozi wao. Rashid Hamisi anafanya hivyo kwa kumhusisha kijana Swaleh katika ulanguzi wa madawa ya kulevya ambapo soko lake lengwa lilikuwa ni vijana.

### 4.3. Umaskini

Umaskini katika taifa hupimwa kulingana na uwezo wa kifedha na hasa kiasi cha matumizi ya wastani ili kupima kiwango cha mapato. Kulingana na viwango vya kimataifa, iwapo familia haina uwezo wa kugharamia matumizi ya dola moja kwa siku basi familia kama hiyo ni maskini. Katika taifa letu la Kenya, asilimia kubwa ya wananchi huishi chini ya kiwango hiki na kwa hivyo wanaweza kuchukuliwa kama maskini. Jambo hili linasababishwa na ugavi mbaya wa raslimali za kitaifa ambao hauna usawa na ndipo ikadaiwa kwamba taifa la Kenya lina mamilionea kumi kati ya mamilioni ya watu maskini. Hali hii inadhihirishwa na ukweli uliopo ambapo watu wachache wanamiliki mamilioni na mamilioni ya ekari za mashamba pamoja na raslimali zingine kama majumba ya kifahari mijini huku wananchi wengi wakiwa ni maskwota wasiokuwa hata na nukta ya ekari ya kujivunia.

Zamani kabla hali ya ubinafsi kumea mizizi katika nchi yetu, hasa kabla ya majilio ya wakoloni, tatizo la umaskini miongoni mwa vijana halikuwepo kwa sababu mbali na ukweli kwamba umiliki wa mali katika msingi ya utamaduni ulikuwa ni wa kikoa huku mali ikiwa ni ya umma, kulikuwa vilevile na uhakika wa kurithi mali katika familia au jamii fulani. Kwa wakati huu, mambo ni tofauti kabisa kiasi kwamba vijana wengi hawana matumaini ya kurithi chochote kwa sababu hata wazazi wao vilevile hawana chochote cha kuwarithisha. Hali hii ilichangiwa na mambo mengi sana. Kwanza kabisa ni tukio la ukoloni ambalo lilileta sera ya ubinafsishaji wa umiliki kwani walowezi hao walipofika sehemu hizi walinyakua ardhi kubwa kutoka kwa wenyeji. Wakati wa uhuru Wafrika waliochukua hatamu za uongozi wakarithi mali kutoka kwa wakoloni hao bila kujali maslahi ya wale wenzao ambao

mashamba yao yalichukuliwa wakati huo wa ukoloni. Mwishowe ardhi tele ikawa mikononi mwa wachache huku asilimia kubwa ya wananchi ikibaki maskini. Hili ni tatizo ambalo Tume ya Haki na Maridhiano inajaribu kukabiliana nalo kwa misingi ya dhuluma na uonevu wa kihistoria nchini mwetu.

Tatizo lingine ambalo linachangia kuongezeka kwa hali ya umaskini nchini ni ongezeko la haraka la idadi ya watu. Kulingana na tarakimu za sensa wakati wa kunyakua uhuru wetu mwaka wa 1963, idadi ya watu nchini Kenya ilikuwa ni milioni nane tu. Miaka 50 baadaye idadi hii imeongezeka zaidi ya mara tano kumaanisha kwamba kila baada ya miaka kumi idadi ya watu inaongezeka kwa zaidi ya watu milioni tano. Jambo hili linaweka shinikizo kubwa sana kwa raslimali chache zilizopo kwa sababu eneo la ardhi linabaki ni lilelile. Hata pale ambapo urithi wa mali kama ardhi uliwezekana katika familia miaka ishirini iliyopita, hili haliwezekani kwa sasa kwa sababu ya kupunguka kwa ukubwa wa kipande chenyewe cha ardhi ambapo kimekatwa hadi kufikia kiasi ambacho hakiwezi kukatwa tena. Hata kilimo katika vijisehemu kama hivyo hakina manufaa tena. Isitoshe baadhi ya vijana hawa wamezaliwa katika sehemu za mijini, huku wazazi wao vilevile wakiwa ni wazaliwa wa mijini hata wasiokuwa na shamba la ukoo la kumiliki popote nchini.

Katika hali kama hiyo vijana wanaridhi umaskini ambao aghalabu utaendelea kudumu katika familia. Hali hii si ya kubuni wala kifantasia kwani ndiyo iliyokidhiri katika makao mengi ya mabanda katika jiji la Nairobi kama vile Mathare, Korogocho, Kibera, Mukuru na mitaa mingine mingi ya aina hiyo. Matokeo ya hali hii ni kwamba vijana huingilia unywaji wa pombe haramu na vileo vingine na hatimaye kutumbukia katika uhalifu. Baadhi ya vileo huathiri vijana sana kiafya hivi kwamba utamuona kijana wa umri mdogo wa miaka ishirini na mitano anayeonekana mkongwe zaidi kuliko ule umri wake. Kwa ajili ya ukosefu wa fedha hata elimu nzuri ni shida kupatikana kwa wazazi hawawezi kuigharamia.

Katika *Vipanya vya Maabara,* umaskini umedhihirika katika familia yao Bob ambapo hata kabla ya babake kuvunjika moyo na kuingilia unywaji wa pombe kupindukia, hali yake kifedha ilikuwa ni ya kusikitisha kwa sababu hata mshahara alioupata haukumwezesha kuyakidhi mahitaji yote ya familia. Hali ya lishe katika familia hiyo ilikuwa mbovu ambapo mara nyingi kiasi kidogo cha pesa alichompa mkewe kuendesha mahitaji ya nyumbani kiliisha hata kabla ya mwezi kuisha. (uk 32) Ilikuwa ni nadra sana kwao kula nyama katika familia. (uk 29) ……*chajio kilikuwa ugali na kitoeo cha karoti na kabeji. Hakikuwa kibaya wala kizuri* ……….. Umaskini huu uliendelea kuibana familia hiyo hata zaidi hasa baada ya Konstebo Kerogo kuingilia unywaji wa pombe.

Elimu ya vijana hao Bob na Freda iliathirika sana kwa ajili ya ukosefu wa fedha za kuwalipia karo na ikabidi mama yao kuombaomba kutoka kwa nduguye Mbaabu ili kuwalisha na kuwaelimisha. Umaskini kutokana na mishahara ya chini katika familia vilevile uliathiri vijana wengine kama Swaleh na Wairi kwa sababu wazazi wao walilazimika kutumia muda wao mwingi wakitafuta fedha zaidi kulijaza pengo ambalo lilisababishwa na mishahara yao midogo. Kwa sababu hii vijana hao walikosa mwongozo wa wazazi wao na kushauriwa ipasavyo. Katika umri wake huo mdogo ilimlazimu Bob kugharamia ununuzi wa chakula nyumbani alipojaliwa kupata pesa kidogo kutokana na vibarua alivyofanya.

### 4.4. Ukosefu wa Ajira

Ukosefu wa ajira ni miongoni mwa matatizo makubwa sana yanayoikumba nchi yetu. Hali hii ndiyo inayosababisha kuongezeka kwa uhalifu. Vijana wengi sana ambao wanakaa bure bila kazi huwa na ushawishi wa kujiingiza katika uhalifu ili wajipatie riziki yao ya kila siku. Hata makundi mengi haramu nchini kama vile *Mungiki* yanazuka kutokana na matatizo ya kiuchumi ambayo yanawapata vijana hao kutokana na ukosefu wa ajira. Katika kutambua hatari iliyopo nchini ikiwa vijana hawana ajira, serikali mnamo mwaka wa 2010 ilianzisha

mpango wa *Kazi kwa Vijana* ambapo lengo lake lilikuwa ni kubuni nafasi za kazi katika kila eneo Bunge ili kujaribu kukabiliana na tatizo hilo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Lakini kutokana na mipango mibaya ya kuanzisha miradi yenyewe bila kufanya utafiti kwanza, pamoja na hali ya ufisadi, mpango hiyo ilikosa kufaulu kwani vijana hufanya vibarua vya muda kama vile kufyeka kando kando ya barabara ambapo mapato duni waliyolipwa yaliifanya hali yao kuwa hata mbaya zaidi.

Tatizo la ukosefu wa ajira linatokana na mipango mibaya kutoka kwa serikali yenyewe. Tatizo hili linatokana na mfumo wa elimu ambao una matatizo chungu nzima. Tatizo la kwanza ni msisitizo mkubwa unaowekewa kupita mtihani iwe katika darasa la nane, kidato cha nne au hata katika vyuo vikuu. Watoto wanaelekezwa kusoma kikasuku ili wapite mitihani lakini hawana ujuzi wowote wa kujitegemea hata baada ya kuipita mitihani yenyewe. Katika darasa la nane, wale ambao hawafaulu hupita mtihani huo wa K.C.P.E na kujiunga na kidato cha kwanza huishia vijijini au hata mijini bila matumaini kwa sababu hawana ujuzi wowote wa kutumia ili kujitegemea maishani. Hali ni ile ile katika kidato cha nne ambapo wale wasiopita mtihani wa K.C.S.E na kujiunga na vyuo vikuu hujikuta katika hali ile. Badala ya mafunzo au masomo haya ya jumla ambayo wanafunzi wanayasoma kikasuku kwa ajili ya kupita mtihani, jitihada zingefanywa ili kugundua talanta zao mapema maishani ili kusomea zile taaluma ambazo zinawafaa.

Tatizo hili la ukosefu wa ajira pia limechangiwa na mifumo ya elimu na kozi katika vyuo vikuu. Kwanza vyuo vikuu vyenyewe vimekuwa ni kama vituo vya kufanyia biashara ambapo kila chuo kinajitahidi kuwasajili wasomi wengi iwezekanavyo ili kupata fedha zaidi. Mbali na vyuo vikuu vya umma ambavyo vinaendelea kupanuliwa kila uchao kwa kufunguliwa vitivo vingi nyanjani hata vile vya kibinafsi vinaendelea kusajiliwa kila mahali. Ni kama kuna uazimu wa kila mtu kupata shahada ya digrii nchini. Katika hali hii ya

kukanganya, vyuo hivi vimetoa wasomi wenye shahada za digrii ambazo hazina manufaa yoyote kwa taifa katika taaluma ambazo hazina hata nafasi za ajira kwa vijana kama hao. Baada ya kutumia pesa nyingi kwa masomo yao ili kupata digrii hizo na hatimaye kukosa ajira vijana huishia katika hali ya kukata tamaa na hivyo kujazwa hasira ambazo zinawaingiza katika visa vya uhalifu. Masomo yamegeuzwa na kuwa biashara ambayo inachangia hata zaidi tatizo la ukosefu wa ajira.

Suluhisho limo katika kuwapa vijana mafunzo ya kuwawezesha kujiajiri wenyewe na hivyo hata kuweza kubuni nafasi za ajira kwa wengine badala ya kazi zile ambazo zinawaacha wasomi kwa kazi za kuajiriwa afisini kwani kazi kama hizo hazipo. Baadhi ya sera za serikali vilevile zinachangia sana kuzidisha tatizo ili hili. Kwanza kabisa ni ule uamuzi ambao serikali ilichukua wa kuongeza umri wa kustaafu kwa wafanyikazi wa umma kutoka miaka hamsini na mitano hadi sitini. Uamuzi huo uliwafungia nje vijana wengi ambao wangezichukua nafasi zilizoachwa na wazee waliostaafu. Ikumbukwe kwamba kila mwaka kuna vijana wengi sana ambao wanafuzu kutoka taasisi mbalimbali na hata vyuo vikuu.

Kwa hivyo baada ya miaka mitano kutakuwa na idadi kubwa sana ya vijana wanaotafuta ajira. Kunalo vilevile tatizo lingine kubwa sana la kutuama kwa ustawi wa viwanda ambavyo vingetoa nafasi ya ajira kwa vijana. Kwa wakati huu serikali yetu inaagiza bidhaa nyingi sana kutoka nchi za kigeni vikiwemo viatu na nguo za mitumba pia. Hata magari yaliyotumiwa huagizwa kutoka nje. Katika hali hii ya kuagiza kila kitu kutoka nje, nafasi za kazi haziwezi kubuniwa, badala yake huwa zinazidi kudidimia. Kwa hivyo serikali ni lazima ibuni sera mpya kuhusu ufunguzi na upanuzi wa viwanda vyake ili kukuza nafasi za kazi kwa vijana wake, lau sivyo hali itaendelea kuwa hata mbaya zaidi.

Tatizo la ukosefu wa ajira limeangaziwa katika *Vipanya vya Maabara* ambapo msanii anatoa mfano wa hali ya kusikitisha sana ambayo inavyokabili vijana wanaotafuta ajira katika viwanda vya Wahindi vilivyopo eneo la viwanda jijini Nairobi. (uk 103)……. *vibarua vya kule industrial area vilikuwa vimenishinda. Vilikuwa vigumu mno na malipo yake yalikuwa duni* ……….Kila asubuhi vijana hawa hurauka na kutembea mwendo mrefu sana hadi sehemu za viwanda . Wengine hutoka umbali wa zaidi ya kilomita kumi. Wafikapo katika majengo ya viwanda hivyo, wao hupiga foleni wakiwa na matumaini ya kupata ajira lakini ni wachache tu wanaochaguliwa na Wahindi hao kwa njia ya kiburi huku wengi wakibaki katika hali ya kukata tamaa. Isitoshe malipo ambayo wanapewa baada ya kazi za sulubu za mchana kutwa ni ya kusikitisha vilevile ni kama hali ya utumwa.

Bob Kerogo vilevile ametumiwa kama kielelezo cha tatizo hili la ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana. Baada ya wanafunzi hao kukamilisha masomo yao ya kidato cha nne bila ya kupata ujuzi wowote, wanabakia kufanya vibarua ambavyo havihitaji elimu yoyote kama vile uoshaji wa gari au hata kupanga vitabu katika rafu dukani kama alivyofanya Bob katika duka lake yule Mhindi Devji. Kuna wengine ambao wanaingilia uhalifu kama vile Swaleh. Ukosefu wa ajira ni tatizo nyeti sana miongoni mwa vijana. Serikali ni lazima itafutie suluhisho la haraka kwani isipofanya hivyo inaweza kuleta madhara makubwa kwa taifa. Vijana ambao wamepoteza matumaini ni tishio kubwa sana kwa usalama wa nchi. Hali hii huenda ikawa hali mbaya sana katika serikali hii ya ugatuzi kwa sababu kuna Kaunti zingine ambazo hazina hata viwanda vya kuweza kuwaajiri vijana wao.

### 4.5. Ukosefu wa Maadili

Katika jamii za kiasili ambapo utamaduni ulithaminiwa, vijana walifunzwa maadili katika jamii. Wavulana walifunzwa na baba zao huku wasichana walifunzwa na mama zao. Katika mambo ya kimapenzi, vijana walionywa dhidi ya kujiingiza katika visa vya ngono na hasa

wasichana ambao kwa bahati mbaya walipata mimba nje ya ndoa waliwaletea wazazi wao aibu kubwa na aghalabu wangeolewa na wazee. Vijana walihimizwa kutohusiana kimapenzi na wenzao majirani hata kama hawakuwa ni wa jamaa moja. Ujirani huo uliwafanya wajione kama ni ndugu na dada na hivyo kuepukana kabisa na visa vyovyote vya mapenzi au ngono baina yao. Kuporomoka kwa kiwango cha maadili katika jamii kimesababishwa na mambo mengi. Kwa mfano, kuporomoka kwa mifumo ya utamaduni katika mipangilio ya familia kumechangia hali hii. Zamani watu waliishi vijijini kama familia moja ambapo watoto wangepata ushauri kutoka kwa wazazi wao. Hata wajukuu wangepewa mawaidha muhimu na nyanya au mababu zao. Hali hii imebadilika kwa sababu watoto wanapata nafasi ndogo ya kukaa na wazazi wao ili washauriwe kwa sababu muda wao mwingi huwa wako shuleni.

Jambo lingine ambalo linachangia sana kuzorota kwa maadili ni athari za mitandao inayowezesha vijana kuona na hata kuiga maadili ambayo haiambatani na utamaduni wa Mwafrika. Baadhi ya mambo haya ni kama vile matumizi ya madawa ya kulevya na hata mapenzi baina ya watu wa jinsia moja kama vile usagaji na ubasha. Mambo kama hayo yalichukuliwa kama miiko na yaliadhibiwa vikali kwa wale ambao walipatikana wakijiusisha na tabia kama hizo. Nidhamu ilikuwepo kwa sababu kulikuwa na mwongozo uliotolewa katika jamii ili kuhakikisha kwamba maadili bora yamezingatiwa.

Siku hizi mambo yamebadilika sana hivi kwamba hata pale ambapo serikali itataka kutoa mwongozo kwa wananchi wake; kuna wale ambao watakimbia kortini wakidai kwamba haki zao za kibinafsi zinakiukwa. Uhuru huu wa mtu binafsi ndio unaovuruga maadili katika jamii na ndipo hata wasichana wataonekana wakitembea nusu uchi kwa sababu ni haki yao kufanya hivyo na yote haya yanatokana na kuiga mambo ambayo wanayaona kwenye mtandao. Athari za mtandao ni kubwa sana kwa vijana wetu na iwapo serikali haitaweza kusimama kidete na kutoa mwongozo basi hali hii itazidi kuzorota. Jambo la kusikitisha ni kwamba hata uongozi

wenyewe mara nyingi huwa unazua hali ya kutatanisha. Hivi majuzi kumekuwa na kisa kimoja kumhusu waziri wa elimu ambaye aliunga mkono wanafunzi wa shule fulani ya upili ambao waligoma kwa sababu wliitaka waruhusiwe kuvaa miniskati au skati fupi sana. Hali kama hii kwa hakika ni ya kusikitisha na inahitaji mwongozo bora ambao unafaa kufuatwa na vijana. Ni muhimu kwa taifa kuwa na mwongozo fulani unaohusiana na maadili.

Katika *Vipanya vya Maabara* tunaona mifano hii ambapo watoto wanakosa maadili. Kwa mfano, wakati wa kuadhimisha mwaka wake wa kumi na sita wa kuzaliwa, Wairi aliandaa dhifa nyumbani kwao akawaalika marafiki zake lakini hata wazazi wake hawakuwa karibu. Uhuru kama huu kwa mototo msichana wa umri huu unaonyesha utovu wa maadili. Isitoshe kulikuwa na mwakilishi wa mwalimu mkuu ambaye alileta zawadi ya shilingi mia tano. Si vyema kwa mtoto wa shule kukubali kufanya mapenzi na mwalimu mkuu wa shule. Badala yake mtoto mwenye nidhamu angewafahamisha wazazi wake kuhusu jambo kama hilo.

Uhusiano wa kimapenzi baina ya vijana hao hao vilevile ulibainisha ukosefu wa maadili. Wakiwa katika shule ya msingi ya Uhuru tayari walikuwa wameunda "jozi za kimapenzi" kama vile Muli na Wairi, Bob na Jamila, Okach na Freda, Swaleh na Achieng na kadhalika. Miongoni mwa vijana ambao walithamini maadili, uhusiano kama huu haungezuka kwa sababu wangejiona kama ndugu na dada. Lakini badala yake walijihusisha na mapenzi baina yao yamkini kwa sababu ya kutoelekezwa na kushauriwa na wazazi wao kuhusu uadilifu katika mahusiano. Kwa hakika, lilikuwa ni tukio la kushangaza na kusikitisha mno kwa msichana kama Jamila atumie fursa ya wazazi wake kutokuwa nyumbani kumleta mvulana chumbani mwake ili kufanya mapenzi naye na hata kufurahia kuupoteza ubikira wake ......(uk 62) ........ *polepole wazimu wa mapenzi ulitupeperusha hadi kwenye kitanda. Kwa muda tuliketi pembeni na kupapasana* ........ Kama ilivyosemekana hapo awali ilikuwa ni muhali sana kwa wasichana kupata mimba nje ya ndoa katika maisha ya kitamaduni. Lakini

tunamshuhudia msichana Wairi akizaa akiwa katika kidato cha pili. Isitoshe alimwachia mamake mtoto huyo na kuhamia mjini ili kuwa kahaba. Aliyafanya yote hayo bila haya, ikiwa na maana kwamba kiwango chake cha maadili vilevile kilikuwa ni cha chini mno. Bob kwa upande wake vilevile anadhihirisha utovu wa maadili kutokana na uhusiano wake wa kimapenzi. Anafanya ngono ovyo ovyo bila kujali athari yake. Anajihusisha kimapenzi naye Jamila, Vera na hata Gaceri. Waziri Rashid Hamisi alidhihirisha hata zaidi upotofu wa maadili kwa kumbaka bintiye Seneta Humphrey King na kisha kumwua.

### 4.6. Maradhi ya Ukimwi

Ukimwi ni kifupisho cha Ukosefu wa Kinga Mwilini (yaani A.I.Ds). Hii ni hali ambayo inatokea baada ya mhasiriwa kuambukizwa na viruzi hivyo vinavyoitwa (H.I.V) na ambavyo hushambulia mwili kwa kuondoa nguvu za mwili ili usiweze kupambana na magonjwa. Virusi hivi hushambulia chembechembe za damu ambazo zinahusika na kuukinga mwili dhidi ya maradhi mbalimbali. Hadi sasa hakuna tiba yoyote ambayo imevumbuliwa ili kukabiliana na ugonjwa wenyewe ingawa kuna madawa yanayotumiwa ili kupunguza makali ya maradhi hayo. Madawa haya yanayoitwa A.R.V's kwa kifupi huwa yanasaidia kupunguza makali ya virusi hivyo ili kumwezesha mhasiriwa kuishi kwa muda mrefu zaidi. Magonjwa haya yanasambazwa sana kupitia kwa ngono ingawa mtagusano na damu ile ambayo ina virusi hivi huweza kuambukiza. kwa mfano kutokana na kujikata kwa kisu ambacho tayari kimemkata mtu ambaye ana maradhi hayo.

Serikali inafanya juhudi kubwa sana ili kuwahamasisha watu kuhusiana na maradhi hayo. Kwa mfano watu wameonywa wajihadhari na kufanya mapenzi kiholela. Hata serikali imehamasisha jamii zile ambazo haziwatahiri wanaume kufanya hivyo kama njia moja ya kukabiliana na maradhi hayo. Katika *Vipanya vya Maabara,* Wairi ni mhasiriwa wa ugonjwa huu kwa sababu katika shughuli zake za ukahaba baadhi ya wateja wake hawakutumia kinga

yoyote na ndipo akaambukizwa na hatimaye kufa. Kwa hakika maradhi ya ukimwi ni tisho kubwa sana kwa vijana na ni muhimu wafanye hathari ili kuepukana nayo lau sivyo ugonjwa huo utawaangamiza.

**4.7. Ufisadi**

Kamusi ya TUKI (2005) inaelezea ufisadi kama uharibifu au matendo mabaya. Neno lenyewe linatokana na kitenzi fisidi ambacho kamusi hiyo inakitafsiri kama kufanya uharibifu au kutumia kwa njia mbaya . Maelezo haya ni ya jumla. Tungependa kuongezea ufafanuzi huu kwa kuelezea ufisadi kama utendaji kazi kwa njia ambayo haina uadilifu na hivyo kuleta athari hasi katika jamiii. Nchini Kenya swala la ufisadi limejitokeza kama tatizo nyeti la kukera taifa zima. Katika miaka ya tisini kulikuwa na sakata ya Goldenberg ambayo ilisababisha serikali kupoteza mabilioni ya fedha kupitia mipango bandia na ghushi ya ununuzi wa madini. Ufisadi hujitokeza si katika upunjaji na ufujaji wa fedha za umma bali pia katika uajiri wa wafanyikazi katika taasisi mbalimbali. Tatizo la ufisadi nchini Kenya ni sugu sana hivi kwamba serikali imewajibika kubuni tume ya Maadili na Vita Dhidi ya Ufisadi (EACC) inayohusiana na kutathmini maadili miongoni mwa umma.

Riwaya hii imeliangazia tatizo hili. Konstebo Kerogo alihudumu kwa muda mrefu kama polisi wa kawaida bila kupandishwa cheo hata mara moja. Watu waliajiriwa baada yake kama vile Inspekta Igweta, Okoth, Swaleh, walipandishwa vyeo na yeye akabaki palepale kwa sababu ya uwazi wake. Jambo hili lilimsukuma Konstebo kuvunjika moyo na kuingilia ulevi, (uk 27-28) "*.......kweli mwanangu lakini leo, orodha ndefu ya polisi walipandishwa cheo.......jina lake halikusomwa.*" Katika ulevi wake Konstebo Kerogo anadai kwamba ufisadi na mapendeleo yamekithiri (uk 30).

Mbali na mapendeleo katika upandishaji vyeo, kuna aina nyingine ya ufisadi unaohusiana na polisi kukodisha bunduki zao kwa majambazi ili zitumike katika visa vya unyang'anyi huku wakipokea malipo kwa kila operesheni. Mfano mzuri ni wa polisi Kamash ambaye alikodisha bunduki yake kwa vijana majambazi kama Swaleh na Kariuki kutekeleza visa vya unyang'anyi. Wananchi nao vilevile wanaonyesha kuficha ufisadi. Wakati Senata King alifika nchini mara ya kwanza ili kuchunguza mauaji ya bintiye, palifunguliwa kituo ambacho kilitumiwa kuwapata watu wenye ushahidi au habari za kuaminika kuhusiana na mauaji hayo. Lakini kwa ajili ya ufisadi mashahidi wengi bandia walifika katika kituo hicho kwa madai ya kutoa ushahidi ili wapate shilingi mia tano zilizotolewa. Baadaye maafisa hao waligundua kwamba wengi waliofika mahali hapo walikuwa ni waongo waliotaka kujinufaisha tu (uk 196).

Hali ya viongozi kujinufaisha na ulanguzi wa madawa ya kulevya ni aina ya ufisadi kwa sababu lengo la kuuza madawa ya kulevya ni kujitajirisha kwa mbinu haramu. Isitoshe hali hii inakuwa hata mbaya zaidi iwapo madawa hayo yanawalenga vijana. Mara nyingi viongozi kama hawa hukingwa na sheria ili maovu yao yasigunduliwe. Waziri Rashid Hamisi anawaingiza vijana kama Swaleh katika biashara ya kuuza madawa hayo. Soko lengwa la kuuza madawa hayo lilikuwa ni vijana katika sehemu mbali mbali za starehe.

**4.8. Vijana kutumiwa kama Vipanya vya Maabara.**

Anwani ya kitabu hiki vilevile imebeba ujumbe muhimu. Vipanya vya Maabara ni aina maalumu wa panya wanaofugwa katika maabara kwa lengo la kufanyiwa utafiti hasa katika majaribio ya tiba. Vipanya kama hivyo hupewa Kemikali au dawa ile inayofanyiwa majaribio ili kukadiria ufanisi wake au hata athari zake. Madaktari au wanasayansi huwa hawajali kamwe maisha ya vipanya hivyo. Lengo lao muhimu ni kuthibitisha utendaji kazi wa dawa ile kwani baada ya jaribio fulani na matokeo kuandikishwa, vipanya hivyo vinaweza

kuangamizwa makusudi na wanasayansi hao. Jinsi wanasayansi wanavyotendea vipanya ndivyo viongozi wanavyowatendea vijana.

Mifano mbalimbali ya majaribio haya yameangaziwa katika *Vipanya vya Maabara*. Kuna majaribio ya mfumo wa elimu wa 8-8-4 ambao umetekelezwa kwa vijana bila kufanyiwa majaribio ya kutosha kwanza ili kuthibitisha ufaafu wao. Hatimaye vijana wengi kama Bob wanapokamilisha mafunzo yao wanajikuta bila ajira kwa kukosa ujuzi unaofaa. Kunayo pia majaribio ya kiuchumi kama vile mpango wa serikali kupunguza gharama. Gacheri alikuwa ni mhasiriwa wa jaribio hili. Aliachishwa kazi mahali alipokuwa akifanya. Baadaye alikumbwa na matatizo mengi ya kujikimu maishani hata ikamlazimu kutafuta mkopo kutoka kwake Bob hapo baadaye. Majaribio ya aina hii yanachangia kuongezeka hata zaidi kwa vijana ambao hawana ajira.

### 4.9. Vijana kama msingi wa kubomoa ukabila

Ukabila ni mojawapo ya matatizo nyeti yanayolikumba taifa la letu. Tatizo hili limejitokeza si katika vyama vya kisiasa tu bali pia katika uteuzi au uajiri wa watu kazini ambapo mtu fulani mashuhuri akiwa mamlakani yeye hufikiria tu kuwaajiri watu kutoka kabila lake. Kitendo hiki kinaonyesha mapendeleo ya kikabila na vile vile ufisadi. Katika siasa watu vilevile huwaunga mkono na kuwapigia kura watu wa kabila lao. Hisia za ukabila ziliibuka kwa nguvu zaidi kufuatia uchaguzi wa utata wa 2007 na vurugu lililofuatia 2008. Aghalabu, viongozi ndio huzipanda mbegu za ukabila miongoni mwa wale wanaotaka wawapigie kura. Hata sasa huku kura zikitarajiwa kupigwa mwaka 2013, tayari kuna tetesi nyingi kuhusu makabila makubwa na madogo.

Katika *vipanya vya maabara* vijana wanaonyesha utangamano na mshikano wa dhati bila kujali kabila. Wakati wa shida na raha, vijana hao huonyesha muumano usio na kifani. Kwa

mfano wakati Wairi alipoandaa dhifa ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa akiwa katika kidato cha pili, marafiki zake wote kutoka makabila mbalimbali nchini walihudhuria bila kujali kabila lolote binafsi. Hivyo ndivyo ilivyokuwa hata wakati wa kifo chake. Marafiki wake wote walihudhuria hata wakati wa kufuzu kwake Freda hafla yake ilihudhuriwa na marafiki hao wote.

### 4.10. Hitimisho

Katika sura hii inabainika vile vile kwamba wazazi wanachangia pakubwa shida hizi zinazowakumba vijana. Endapo wazazi watatoa mchango wao ipasavyo, vijana watapata msingi unaofaa kuwapa matumaini na uthabiti maishani. Licha ya shida hizi bado wanadhihirisha mambo mengi chanya. Hawaonyeshi tu mshikamano wa kuondoa ukabila bali pia wanajitokeza na mbinu mwafaka za uwekezaji ambazo zinaondoa hali ngumu ya uchumi.

Kila taifa linahitaji kizazi kijacho ambacho kinaweza kuwekewa matumaini. Hali hii inatokana na serikali na viongozi kuyawekea kipa umbele maslahi ya vijana katika jamii kwa sababu wasipofanya hivyo taifa litakosa msingi dhabiti wa viongozi wa siku zijazo. Kwa hivyo ni muhimu kwa serikali kufanya kila juhudi kuhakikisha kwamba maslahi ya vijana yanaangaliwa. Baadhi ya hatua ambazo serikali inafaa kuchukua ni kuhakikisha kwamba imeweka sera kabambe kuhusu elimu na ajira ya vijana na jambo hili lifuatiliwe mfululizo kwa kipindi cha angalau miaka kumi ili kutathmini ufanisi wake. Kwa kufanya hivyo serikali itakuwa na uhakika kwamba taifa litaendelea kuimarika katika nyanja zote.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO LA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunawasililisha hitimisho la utafiti wetu ambao madhumuni yake yalikuwa ni kuchunguza changamoto zinazowakumba vijana pamoja na kutathimini kiini cha matatizo hayo. Vilevile utafiti huu ulilenga kubainisha namna vijana wanavyoweza kuchangia katika kubomoa ukabila. Sura hii imeshughulikia matokeo ya utafiti wetu kwa mujibu wa madhumuni yetu pamoja na nadharia tete zilizotokana na madhumuni hayo. Ili kuweza kuyatimiza hayo yote tumegawa kazi hii katika sura tano ambapo sura ya kwanza imebeba tatizo au somo la utafiti, sura ya pili imebeba dhana ya uhusika pamoja na aina mbalimbali za wahusika. Sura yetu ya tatu imebeba uhakiki wa wahusika, nayo sura ya nne imebeba uhakiki wa maudhui, hatimaye sura ya tano imeshughulikia hitimisho letu.

### 5.1. Matokeo ya Utafiti.

Kutokana na maudhumuni pamoja na nadharia tete zilizopendekezwa kuhusiana na utafiti wetu matokeo kadhaa yalibainika. Kwanza kuhusiana na changamoto zinazowakumba vijana, ilibainika kwamba matatizo ya kiuchumi yanachangia pakubwa jambo hili. Wazazi wengi hukosa nafasi ya kukaa na wanao na kuwaelekeza kwa sababu muda wao mwingi hutumiwa kutafuta chumo. Hali hii huwafanya vijana kutoka familia kama hizo kukosa maelekezi na hata mfano mzuri wa kuiga. Mbali na hayo kunao wazazi wengine ambao hutaka kuwapa wanao masharti magumu ya kutaka wasitangamane na vijana wenzao kwa misingi fulani ya kijamii kama vile dini. Mambo kama haya huwafanya vijana hao wanaotawishwa kupata hamu ya kukiuka yale masharti ambayo wazazi wao wanawashuritisha kuzingatia.

Tuligundua vilevile kwamba serikali inachangia sana matatizo yanayowakumba vijana kutokana na baadhi ya sera zake mbovu. Miongoni mwa sera hizi ni kama vile kuanzishwa

kwa mfumo wa elimu wa nane nne nne ambao ulitekelezwa bila kufanyiwa majaribio ya kutosha ili kubainisha ufaafu wake. Mwishowe, vijana wengi wanaopitia mfumo huu hujikuta katika tatizo la ukosefu wa ajira kutokana na kutokuwa na ujuzi unaotakikana.

Sera nyingine inayoathiri vijana ni ile ya kupunguza gharama. Katika sera hii serikali huwaachisha waajiriwa kazi kwa lengo la kupunguza gharama. Vijana kama hao wanaachishwa kazi hizo hubakia katika hali ya kutamausha. Kutokana na hayo serikali inawatumia vijana kama vipanya vya maabara vya kufanyiwa majaribio na sera hizo. Vijana wengi wanakabiliwa na tishio la kuangamia endapo serikali haitingilia kati na kubuni mikakati ya kuwaokoa kwa kuangazia matatizo yanayowakumba kwa wakati huu. Baadhi ya vifo hivi vinavyowakabili mapema maishani mwao vinatokana na uhalifu au maradhi ya ukimwi. Sababu zote hizi zinahusiana na shinikizo za kijamii zinazowakumba vijana.

Matokeo mengine muhimu yanahusu nafasi ya vijana katika uangamizaji wa ukabila. Hii ina maana kwamba vijana ndio wana nafasi kubwa zaidi ya kuangamiza ukabila. Vijana wakiwa katika mazingira horomo isiyotiwa cheche za sumu na watu wazima, wao huonyesha ushirikiano, na mwamana bila kujali makabila yao ndipo vijana kama Bob, Swaleh, Wairi, Okach,Jamila na wangineo wanajiona kama watoto wa Nyayo na kutangamana.

### 5.2. Mapendekezo

Kwa utafiti wa baadaye tumependekeza uchunguzi wa fani katika *Vipanya vya Maabara*. Hii ni kwa sababu fasihi ni aina ya sanaa ambayo inatumia maneno ili kubainisha ukweli wa maisha yake binadamu. Kwa vile lugha ndiyo malighafi inayotumiwa, uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi utakuwa si kamilifu bila kuangalia kipengele hiki muhimu cha fasihi. Riwaya hii imesheni ukwasi wa lugha ambao vipengele vyake vinastahili kufanyiwa utafiti.

**MAREJELEO**


Aristotle/Horace/Longinus (1965). *Classical Literary Criticism.* London: Penguin Books.

Bertoncini, E. Z. (1989). *Outline of Swahili Literature*. Leden: E.J. Brill.

Cuddon , J.A. (1995). *Dictionary of Literary Terms & Literary Theory.* London: Penguin Books.

Habwe, J. (2005). *Paradiso*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Katola, E. (2006). *Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike Katika Tamthilia Za Kiswahili*. UoN (Tasnifu ambayo haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau

________________ (1978). *Kichwa Maji*. Nairobi: Vide – Muwa .

Kiango, S. (1992 *Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya*. UoN (Tasnifu ambayo haijachapishwa).

Kimani, N. na Chimerah, R.(2008) *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kithara wa Mberia., (2001) *Kifo Kisimani*.Nairobi: Marimba Publications

________________ (2008). *Maua Kwenye Jua La Asubuhi.* Nairobi: Marimba Publications

Kitula, K. (2008). *Mwongozo wa Utengano*. Nairobi: Sasa Sema.

Lugano, R. (1989). *Mwanamke Katika Riwaya za Kezlahabi.* UoN (Tasnifu ambayo haijachapishwa)

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Foto form.

____________ (2007) *Vipanya Vya Maabara.* Nairobi: Jomo Kenyatta

Foundation

Mbunda, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: E.A.E.P

Mlacha, S. A.K. na Madumula, J.S. (1989).*Riwaya ya Kiswahili.* Dar- es- Salaam: University Press.

Mogambi, K. (1983) *Uhakiki wa Hali ya Wanyonge Katika Riwaya Tatu za S. Mohamed.* UoN (Tasnifu ambayo haijachapishwa).

Momanyi, C. (2006). *Tumaini.* Nairobi: Vide - Muwa

Mohamed, S.A. (1960) *Kisima cha Giningi.* London: Evans Brothers.

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Fasihi.* Nairobi: E.A.E.P.

Mutua, J. (2007). *Mitazamo ya Vijana na Wazee Kuhusu Ukombozi wa Mwanamke Katika Tamthilia Tatu za Kiswahili.* UoN (Tasnifu ambayo haijachapishwa)

Nazareth, P (1978). *The Third World Writer.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Nkonge , G. (2006). *Athari za Udhanaishi Katika Kichwa Maji na Nguvu ya Sala*. UoN. (Tasnifu ambayo haijachapishwa)

Mdee et al (2009). *Kamusi Kamili ya Kiswahili*: Nairobi: Longhorn.

Said, A. M. (1980) *Utengano*. Nairobi: Longhorn.

Syambo, B.na Mazrui, A.(1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Topan, F. (1971). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili.* Dar es

Salaam: O.U.P

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: O.U.P.

Wafula, R.M. na Kimani, N. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (2003) *Kufa Kuzikana*. Nairobi: Longhorn

Wamitila, K.W. (1999) *Nguvu ya Sala*. Nairobi: Longhorn

______________ (2000). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix

______________ (2003). *Pango.* Nairobi: Vide - Muwa.

______________ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia:* Nairobi: Focus Books.

______________ (2006). *Sumu ya Bafe.* Nairobi: Vide - Muwa

______________ (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi: Vide - Muwa

______________ (2008). *Kanzi ya Fasihi; Misingi ya Uchanganuzi wa a Fasihi*. Nairobi: Vide – Muwa.

______________ (2009). *Bina – Adamu.* Nairobi: Phoenix.

Weller, R. & Austin, W.(1986). *Theory of Literature*. London: Harcourt.